SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA VIWANDA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

MHESHIMIWA: BALOZI AMINA SALUM ALI (MBM)

Mei, 2018

YALIYOMO

1 UTANGULIZI:..... 1
2 MWENENDO WA BIASHARA NA VIWANDA DUNIANI 5
2.1 Hali ya Uchumi na Biashara Duniani:..... 5
2.2 Hali ya Biashara Zanzibar..... 11
3 HALI YA VIWANDA: 16
4 UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MIPANGO YA WIZARA KWA MWAKA 2017 – 2018:..... 27
4.1 PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA..... 31
4.1.1 Programu ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara:..... 31
4.1.2 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara..... 34
4.1.3 Programu ndogo ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba 39
4.2 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI..... 41
4.2.1 Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda..... 42
4.2.2 Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali..... 45
4.3 PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA 47
4.3.1 Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji 47
4.3.2 Programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji 52
4.3.3 Programu ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani 55
4.4 PROGRAMU KUU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA 61
4.4.1 Programu ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora 62

4.5 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC): 64
4.5.1 Uvunaji na Usafirishaji Karafuu:..... 64
4.5.2 Bei ya kununulia Karafuu: 65
4.5.3 Uzalishaji wa Mafuta ya Makonyo na Mimea 66
4.5.4 Mradi wa Kukuza Biashara 66
5 CHANGAMOTO:..... 67
6 PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2018 – 2019 69
6.1 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA 75
6.2 PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI 77
6.3 PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA 78
6.4 PROGRAMU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA 80
6.5 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA – ZSTC 81
7 SHUKRANI: 82
8 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2018 – 2019 84
9 HITIMISHO: 87
10 VIAMBATANISHO..... 88
10.1 Kiambatisho Namba1: Mwenendo wa Biashara Zanzibar (2012 – 2017) TZS.MIL. 88
10.2 Kiambatisho Namba 2: Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara: 89
10.3 Kiambatisho Namba 3: Wastani wa Uingizaji wa Chakula Muhimu 90
10.4 Kiambatisho Namba 4: Mwenendo wa Biashara ya Karafuu kwa Mwaka 2012 – 2018. 91

HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA VIWANDA

MHESHIMIWA BALOZI AMINA SALUM ALI, KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019:

1 UTANGULIZI:

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya kupokea, kupitia, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018 - 2019.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuibariki nchi yetu kuendelea kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufika katika Baraza hili tukiwa wazima na afya njema ili tuweze kuiwasilisha na kuijadili bajeti yetu hii.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, ambae pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuiongoza vyema Zanzibar kwa hekima na upendo na kuhakikisha kwamba amani na utulivu wa nchi yetu inaendelea kudumishwa na kuwafanya wananchi kuweza kuendelea kutekeleza shughuli zao za kiuchumi, biashara na uwekezaji. Pia naomba nitoe shukrani zangu

za dhati kwa imani aliyonayo kwangu na kunichagua kuongoza Wizara hii, naomba nimhakikishie mimi binafsi na watendaji wote kuwa tutatimiza wajibu wetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Pia nachukua fursa hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa jitihada zake za dhati anazozichukua za kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu wa Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile kwa kutupa miongozo, maelekezo na michango yake katika maendeleo ya nchi yetu.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukuwa fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, wenyeviti pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa, michango na ushauri mliotupatia kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa programu za Wizara kwa mwaka wa fedha 2017-2018.

6. **Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya bajeti hii yamepitia katika hatua na ngazi mbali mbali za awali ikiwemo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi. Naomba kuchukua fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni kwa kuchambua mapendekezo ya awali ya bajeti hii na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa kujadiliwa na kuidhinishwa.

7. **Mheshimiwa Spika,** aidha, shukurani zangu za pekee zimwendee Naibu Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh kwa msaada na mashirikiano yake makubwa anayonipatia katika kuhakikisha malengo ya Wizara yanafikiwa. Pia nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii, Wakurugenzi na viongozi wote wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara yangu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipatia yaliyosaidia katika utekelezaji mzuri wa majukumu yangu. Nawaomba watendaji wote hawa waendelee kunipa mashirikiano ili kwa pamoja tuweze kuwahudumia wananchi ipasavyo.

8. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako kuwa muundo wa Wizara hii umefanyiwa mabadiliko ambayo yamehusisha uundwaji wa Wakala wa Kusimamia na Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati *(Small and Medium Industrial Development Agency)* pamoja na Tume ya Ushindani Halali wa Kibiashara *(Fair Competition Commission).* Aidha, jina la Wizara yangu limebadilishwa ambapo hapo awali ilikuwa ikijulikana kwa jina la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na sasa inajulikana kwa jina la Wizara ya Biashara na Viwanda kwa tamko la Serikali la mwaka 2018. Mabadiliko hayo yamekuja kwa mashirikiano ya karibu na Baraza lako tukufu lililowezesha kupitisha miswada ya kuanzisha vyombo hivyo muhimu.

9. **Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya bajeti hii yamezingatia nyenzo muhimu zifuatazo:

i. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais, wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein;

ii. Ilani ya CCM ya mwaka 2015 -2020;

iii. Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020;

iv. Mpango wa Ukuzaji Uchumi na Kuondoa Umasikini Zanzibar (MKUZA III);

v. Maelekezo ya Serikali;

vi. Ukomo wa Rasilimali Fedha uliowekwa kwa Wizara;

vii. Mpango Kazi *(Strategic Plan)* wa Wizara; na

viii. Miongozo ya kisera inayosimamiwa na Wizara.

10. Mheshimiwa Spika, pamoja na mazingatio ya hapo juu, utayarishaji wa mapendekezo haya ulizingatia pia matukio mbali mbali yaliyojitokeza ulimwenguni ambayo yamekuwa na athari za moja kwa moja katika mwenendo wa biashara na uchumi duniani. Matukio hayo ni kama vile mwenendo wa uwekezaji duniani, maendeleo ya biashara na fedha na pia masuala ya kisiasa katika baadhi ya maeneo ya dunia.

11. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu hii, nitaanza kwa kufanya mapitio ya jumla kuhusu mwenendo wa biashara duniani, nchi za kanda ya Afrika Mashariki, SADC, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwenendo wa biashara Zanzibar, mapitio ya hali ya viwanda, utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017 /2018,

taarifa za mashirika na taasisi zinazosimamiwa na Wizara, kubainisha changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2017/2018 na hatimae kubainisha mapendekezo ya bajeti kwa programu za Wizara kwa mwaka 2018/ 2019.

2 MWENENDO WA BIASHARA NA VIWANDA DUNIANI

2.1 Hali ya Uchumi na Biashara Duniani:

12. **Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa uchumi na biashara duniani uliongezeka kutoka asilimia 1.3 mwaka 2016 hadi asilimia 4.7 mwaka 2017. Ukuaji huu unatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kuagiza bidhaa katika nchi mbali mbali duniani hasa katika nchi za Asia na nchi zinazoendelea ingawa taarifa zinaonesha mategemeo ya kupungua kwa ukuaji huo kwa mwaka 2018 na kufikia asilimia 4.4 hata hivyo inategemewa kwa ujumla ukuaji huo utakuwa baina asilimia 3.1 na asilimia 5.5. Mchoro Nam. 1 hapo chini unaonesha zaidi.

Mchoro Nam. 1:
Mchango wa Biashara katika Uchumi wa Dunia 2013 – 2017:



Chanzo: limechorwa na WBV kutokana na takwimu za Shirika la Biashara la Dunia – WTO, 2018

13. **Mheshimiwa Spika,** usafirishaji wa bidhaa duniani kwa kipindi cha mwaka 2017 ulifikia **USD 17,198 bilioni,** ambapo ulikuwa ni ongezeko kwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na usafirishaji uliofanyika mwaka 2016. Katika usafirishaji huo, nchi za Ulaya ziliendelea kuongoza kwa usafirishaji wa bidhaa duniani kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya **USD 6,501 bilioni** sawa na asilimia 37.8 ya usafirishaji wote wa bidhaa duniani. Nchi za Asia zilifuatia kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya **USD 5,842 bilioni** sawa na asilimia 34 ya usafirishaji wote. Aidha, nchi za Marekani ya Kaskazini zilikuwa katika nafasi ya tatu kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya **USD 2,377 bilioni** sawa na asilimia 13.8 ya usafirishaji wote.

14. **Mheshimiwa Spika,** Nchi za Mashariki ya Kati zilisafirisha bidhaa zenye thamani ya **USD 961 billioni** (5.6%) na nchi za Marekani ya Kusini zilisafirisha bidhaa zenye thamani ya **USD 583 billioni** (3.4%). Kwa upande wa nchi za Afrika, zimeendelea kutoa mchango mdogo katika usafirishaji wa bidhaa ambapo kwa mwaka 2017 zilisafirisha bidhaa zenye thamani ya **USD 417 bilioni** sawa na asilimia 2.4 za usafirishaji wote.

15. **Mheshimiwa Spika,** Uagiziaji wa bidhaa duniani kwa mwaka 2017 ulifikia thamani ya **USD 17,572 bilioni,** ambapo nchi za Ulaya ziliongoza kwa kuagiza bidhaa zenye thamani ya **USD 6,521 bilioni** sawa na asilimia 37.1 ya uagiziaji wote. Aidha, katika uagiziaji huo nchi za Asia ziliagiza bidhaa zenye thamani ya **USD 5,541 bilioni** sawa na asilimia 31.5, nchi za Marekani ya Kaskazini ziliagiza bidhaa zenye thamani ya **USD 3,285**

bilioni sawa na asilimia 18.7, na nchi za Mashariki ya Kati ziliagiza bidhaa zenye thamani ya **USD 712 bilioni** sawa na asilimia 4.1. Kwa upande wa nchi za Afrika, jumla ya bidhaa zenye thamani ya **USD 534 bilioni** sawa na asilimia 3.0 ziliagizwa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo huo wa usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa duniani katika kipindi cha mwaka 2017 unaonekana katika **Jadweli Namba 1** hapa chini.

Jadweli Nam. 1:
Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa Duniani 2017 (USD bil):

Kanda	Usafirishaji	Asilimia	Uagiziaji	Asilimia
Ulaya	6,501	37.8	6,521	37.1
Asia	5,842	34.0	5,541	31.5
Marekani/ kaskazini	2,377	13.8	3,285	18.7
Mashariki ya Kati	961	5.6	712	4.1
Marekani/Kusini	583	3.4	579	3.3
Jumuiya ya Madola	518	3.0	402	2.3
Afrika	417	2.4	534	3.0
Jumla	**17,198**	**100**	**17,572**	**100**

Chanzo: Shirika la Biashara la Dunia – WTO.

i. Mwenendo wa Biashara baina ya Zanzibar na Jumuiya za Kikanda (EAC na SADC)

16. Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inaundwa na nchi za Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi,

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sudani ya Kusini. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafanya biashara na nchi wanachama wa jumuiya hii. Hali ya biashara inaonesha kwamba katika mwaka 2017, Zanzibar ilisafirisha kwa ujumla bidhaa zenye thamani ya **TZS 145,756.8 milioni** ambapo jumla ya bidhaa zenye thamani ya **TZS 3,850.7 milioni** sawa na asilimia 2.6 ya thamani ya bidhaa hizo zilisafirishwa kwenda nchi jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa nyingi zaidi zilisafirishwa nchini Uganda zikiwa na thamani **TZS 3,793.4 milioni** ambazo ni aina mbalimbali za mashine *(crushed, filling machine na assorted conveyors).*

17. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uagiziaji, Zanzibar iliagiza jumla ya bidhaa za thamani ya **TZS 211,413.2 milioni,** ambapo bidhaa za thamani ya **TZS 1,222.4 milioni** sawa na asilimia 0.6 ya uagiziaji zimetoka Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa zaidi zimeagizwa kutoka Kenya zikiwemo saruji, nguo na mafuta ya kupikia. Hali ya biashara kati ya Zanzibar na Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kama inavyoonekana katika Mchoro namba 2 hapa chini.

Mchoro Namba2:
Mwenendo wa Biashara baina ya Zanzibar na Jumuiya ya Afrika Mashariki 2013-2017



Chanzo: limechorwa na WBV kutokana na Takwimu za OCGS, 2018

18. **Mheshimiwa Spika,** Jumuiya ya **SADC** inajumuisha nchi 16 zikiwemo Zambia, Afrika ya kusini, Angola, Botswana, Namibia, Zimbabwe na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafanya biashara na nchi wanachama wa jumuiya hii. Hali ya biashara inaonesha kwamba katika mwaka 2017, jumla ya bidhaa zenye thamani ya **TZS. 572.8 milioni** ambayo ni sawa na asilimia 0.4 ya usafirishaji wote zilisafirishwa kwenda nchi za SADC ambapo asilimia kubwa ya usafirishaji ni katika nchi ya Zambia na Afrika ya kusini. Takwimu hizi pia zinaonesha kuwa Zanzibar inayo nafasi ya kulitumia vizuri zaidi soko hilo la SADC.

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uagiziaji wa bidhaa katika mwaka huo huo, Zanzibar iliagiza bidhaa

zenye thamani ya **TZS 3,365.9 milioni** kutoka nchi za Jumuiya ya **SADC** sawa na asilimia 1.6 ya uagizaji wote. Nchi ambayo uagizaji ulikuwa mkubwa ni Afrika ya Kusini ambapo Zanzibar imeagiza bidhaa zikiwemo vifaa vya ujenzi na vifaa vya umeme. Hali ya biashara kati ya Zanzibar na Jumuiya ya **'SADC'** ni kama inavyoonekana katika **Mchoro namba 3** hapa chini.

Mchoro Namba 3: Mwenendo wa Biashara baina ya Zanzibar na Jumuiya ya 'SADC' 2013-2017



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, 2018

20. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia takwimu za usafirishaji na uagizaji wa bidhaa kati ya Zanzibar na nchi wanachama jumuiya za kikanda za EAC na SADC, takwimu zinaonesha kuwa Zanzibar imelitumia vizuri zaidi soko la Afrika Mashariki ikilinganishwa na soko la SADC, hivyo, jitihada zinahitajika kulitumia vizuri soko la SADC hasa kwa kuuza bidhaa zetu Afrika ya Kusini.

2.2 Hali ya Biashara Zanzibar

Usafirishaji na Uagiziaji wa Bidhaa:

21. **Mheshimiwa Spika,** Hali ya biashara kwa ujumla inaonesha kwamba Zanzibar imefanya biashara yenye thamani ya **TZS 357,170.2 milioni** kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na biashara ya **TZS 263,322.9 milioni** mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 15. Biashara hiyo ilikuwa ni usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya Zanzibar na uagiziaji wa bidhaa kuja Zanzibar. Bidhaa ambazo Zanzibar ilisafirisha nchi za nje ni pamoja na karafuu, mwani na mazao ya baharini (majongoo na dagaa).

22. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2017, nchi yetu ilisafirisha nje bidhaa zenye thamani ya **TZS 145,756.8 milioni.** Kiwango hicho cha usafirishaji ni sawa na ongezeko la asilimia 20 kwa kulinganisha na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya **TZS 96,234.9 milioni** uliofanyika kipindi cha mwaka 2016. Katika usafirishaji huo, zao la karafuu lilikuwa na thamani ya **TZS 132,310 milioni** sawa na asilimia 90.77 ya usafirishaji wote. Karafuu hii ilisafirishwa katika nchi za Singapore, India na nchi za Falme za Kiarabu (UAE).

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uagiziaji bidhaa, nchi yetu iliagiza bidhaa zenye thamani ya **TZS. 211,413.4 milioni** kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na uagiziaji wa **TZS. 167,088.0 milioni** mwaka 2016. Bidhaa ambazo Zanzibar imeagiza kutoka nchi za nje ni

pamoja na vyombo vya usafiri, bidhaa za elektroniki kama vile kompyuta, simu, bidhaa za nguo n.k. Mwenendo wa biashara umeonesha kuimarika kwa urari wa biashara kwa kupunguza nakisi yake kutoka **TZS 70,853.1 milioni** hadi **TZS 65,656.54 milioni.** Mchoro Nam.4 hapa chini unatoa ufafanuzi zaidi.

Mchoro Namba 4:
Mwenendo wa Biashara Zanzibar
(2012 – 2017) (Tzs Mil.)



Chanzo: limechorwa na WBV kutokana na Takwimu za OCGS, 2018

Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara
(Inter-state Trade Balance):

24. **Mheshimiwa Spika,** biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara inahusisha utoaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania bara na uingizaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar. Biashara hiyo

inahusisha bidhaa za vyakula vikiwemo mchele, mbatata, maharage, vitunguu, tungule na mboga mboga, viazi vitamu, matunda, vitu vya elektroniki, magari, madawa na vinywaji.

25. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha mwaka 2017, Zanzibar ilipeleka bidhaa Tanzania Bara zenye thamani ya **TZS 33,657.7 milioni,** ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya **TZS 84, 760.9 milioni** zilizopelekwa mwaka 2016. Kiwango hicho cha bidhaa ni zile bidhaa ambazo zinapelekwa katika mfumo ulio rasmi wa kiforodha. Hali hii ya kushuka imesababishwa na kupungua kwa upelekaji wa bidhaa hasa magari tokea mwaka 2015 na bidhaa nyengine za viwandani zilizoshindwa kuingia katika soko hilo ikiwemo maziwa, bidhaa za manukato, maji n.k.

Aidha, katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2017, Zanzibar iliagizia kutoka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani ya **TZS 206,482.2 milioni** ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya **TZS 134,059.5 milioni** kwa mwaka 2016. Uingizaji mkubwa kutoka Tanzania bara umetokea katika bidhaa za kilimo, vyakula, vyuma, magari, maji, vinywaji, dawa n.k.

26. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki biashara kutoka Zanzibar kwenda Bara zimeendelea kupungua na hivyo kusababisha urari mkubwa wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ikilinganishwa na mwaka 2016. Hali hii ilitokana na vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru hasa vibali vya ruhusa ya kuingiza bidhaa na kulazimisha wafanyabiashara wajisajili tena Tanzania bara

hali iliyoleta usumbufu kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Mwenendo wa biashara baina ya pande mbili hizi ni kama inavyoonekana katika **Mchoro Nam 5.** hapa chini.

Mchoro Namba 5: Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara: TZS. (Milioni)



Chanzo: limechorwa na WBV kutokana na Takwimu za OCGS, 2018

27. **Mheshimiwa Spika,** hali hii si nzuri kibiashara na Wizara yangu inafanya jitihada kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali kurejesha hali ya biashara iliyokuwepo baina ya Zanzibar na Tanzania bara hasa kuongeza bidhaa zinazosafirishwa kutoka Zanzibar kwenda katika soko la Tanzania bara.

Hali ya Chakula na Bei katika Soko la Zanzibar

28. **Mheshimiwa Spika,** hali ya uwepo wa chakula hapa Zanzibar kwa mwaka 2017 imeendelea kuwa ya kuridhisha.

Takwimu za uingizaji chakula zinaonesha kwamba jumla ya Tani 20,426.0 za mchele, Tani 29,373.0 za sukari na Tani 12,975.0 za unga wa ngano zilikuwepo katika kipindi hicho kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani kama inavyoonekana katika **Mchoro Nam.6** hapo chini.

Mchoro Namba 6:
Wastani wa Uingizaji wa Chakula Muhimu katika Soko la Zanzibar 2017 (Tani):



Chanzo: Wizara ya Biashara na Viwanda, 2018

29. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bei za bidhaa muhimu kama vile mchele, unga wa ngano pamoja na sukari katika soko la ndani zilikuwa za utulivu licha ya kuwepo kwa ongezeko la jumla la bei za bidhaa hizo katika masoko ya dunia. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wa kusimamia bei za bidhaa muhimu (mchele, sukari na unga wa ngano) kwa kuwashirikisha wafanyabiashara wenyewe na kutoa unafuu maalum wa kodi ili wananchi waweze kupata

nafuu ya bidhaa zilizo muhimu hasa katika kipindi hichi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.

30. Mheshimiwa Spika, kwa jumla wastani wa bei za reja reja za bidhaa hizo kwa mwaka 2017 katika masoko ya Zanzibar ni kama zinavyoonekana katika **Jadweli Nam. 2** hapa chini:

Jadweli Nam. 2:
Wastani wa Bei za Reja Reja za Chakula Muhimu katika soko la Zanzibar:

Bidhaa	Julai - Sept	Okt – Dis	Jan – Machi
Mchele	1,200	1,250	1,250
Sukari	1,800	1,850	1,850
Unga Ngano	1,200	1,200	1,200

Chanzo: Wizara ya Biashara na Viwanda, 2018

31. Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia hali ya mwenendo wa bei za chakula muhimu katika masoko ya Zanzibar kama inavyoonekana katika Jadweli la hapo juu, itagundulika kuwepo kwa ongezeko dogo kwa bei ya sukari na mchele katika robo ya Pili. Hatahivyo, bado bei ya bidhaa hizo zimeendelea kuwa za utulivu hivyo kurahisisha maisha ya Wazanzibar ambao waliowengi wapo katika kipato cha chini.

3 HALI YA VIWANDA:

32. Mheshimiwa Spika, moja ya malengo makubwa ya Serikali ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na kuleta maendeleo ya wananchi.

Uchumi wa viwanda utasaidia kurasimisha sekta isiyo rasmi, kupunguza uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje, kujenga mnyororo wa thamani muhimu kwa kuchochea usindikaji wa mali ghafi, kuchochea bidhaa mpya kwa matumizi na masoko mapya ikiwemo bidhaa hai *(organic products),* kuongeza ajira kwa wazanzibari, kuongeza wigo wa walipa kodi na hatimae kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali.

33. Mheshimiwa Spika, Wizara inaifanyia mapitio Sera ya Viwanda ya mwaka 1998 kwa kuangalia malengo mapya na vipaumbele vinavyokwenda sambamba na Dira na MKUZA III ili vilete muendelezo mzuri katika dira itakayofuatia. Maeneo yaliyopewa vipaumbele ni: i) Usarifu wa bidhaa za kilimo, ii) Uchumi wa bahari *(blue economy)* ikiwemo uvuvi na usarifu wa mazao baharini, kilimo cha baharini na uvuvi wa bahari kuu, iii) Viwanda vyepesi *(light manufacturing),* vikiwemo viwanda vya nguo, chumvi, asali, dagaa, madawa na bidhaa za manukato na viungo kwa soko la ndani na nje, iv) Viwanda kwa ajili ya sekta ya Utalii vikiwemo viwanda vya kazi za mkono, mbao na mali asili ya kilimo.

34. Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji kwa viwanda vikubwa kwa mwaka 2017/18 kwa ujumla imeimarika ikilinganishwa na mwaka wa 2016/17. Hali hiyo imetokana hasa na kuimarika uzalishaji katika kiwanda cha sukari Mahonda pamoja na kuendelea vyema uzalishaji katika viwanda vyengine viwili vikubwa vya Zanzibar ambavyo ni kiwanda cha maziwa kilichopo Fumba na Kiwanda cha Unga wa ngano kilichopo Mtoni. Kiwanda cha Sukari

Mahonda kimeimarisha uzalishaji wa sukari kufuatia ukarabati mkubwa wa mitambo na utanuzi wa mashamba ya miwa pamoja na kuanzisha ununuzi wa miwa kutoka kwa wakulima wa nje *(outgrowers).* Katika mwaka huu kiwanda kinatarajia kuzalisha tani zipatazo 8,000 za sukari kutoka tani 4,805 zilizozalishwa mwaka 2016/17.

35. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uzalishaji wa viwanda vidogo vidogo na vya kati hali haikuwa ya kuridhisha kutokana na changamoto mbali mbali ikiwemo uhaba wa malighafi kwa viwanda vya matofali. Kulingana na Sensa ya Viwanda ya mwaka 2012, Zanzibar kuna jumla ya viwanda 2,201 ambavyo vimeajiri watu 10,427. Kati ya hivyo, viwanda 235 vimeajiri kuanzia watu kumi na kuendelea kila kimoja. Viwanda 19 kati ya hivyo 235 ni vya upigaji matofali na usagaji wa kokoto (Mining and quarrying) na viwanda 216 ni vya uzalishaji (Manufacturing) ambavyo husarifu mazao ya kilimo *(Agro- processing).* Viwanda vyengine vinazalisha sabuni za kukogea, mafuta ya mwili *(body lotion),* shampoo pamoja na sabuni za kusafishia sakafu na vyombo vya jikoni na kadhalika. Ili kuwa na uhakika wa hali ya viwanda nchini, Wizara itafanya utafiti wa kina ili kujua halisi ya viwanda.

36. Mheshimiwa Spika, Zanzibar pia ina viwanda vya uzalishaji *(Manufacturing)* ambavyo vimeajiri watu wengi. Viwanda hivyo ni pamoja Kiwanda cha Makonyo na Arki za mimea (Pemba) na viwanda vya maji na vinywaji baridi. Pia vipo viwanda vya ushoni wa nguo vilivyoko Amaan Industrial Park, viwanda vya kusindika mazao ya viungo, maziwa, majani ya chai, manukato, sukari na kiwanda

cha kutengeneza mifuko ya karatasi. Viwanda vyote hivi vinaendela na uzalishaji wa bidhaa kama kawaida. Kati ya viwanda hivyo vinavyofanya kazi, 18 viko chini ya ZIPA ambako pia miradi mipya mitatu inaendelea na hatua za ujenzi na maombi ya miradi mingine ya kuanzisha viwanda vitano imeshaidhinishwa na ZIPA na inatarajiwa kuanza hatua za ujenzi ndani ya mwaka huu.

37. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa nchi yetu inafanikiwa katika sekta ya viwanda, Wizara imekuwa ikichukua hatua mbali mbali mbali kwa kushirikiana na wadau tofauti. Uundwaji wa Wakala wa Kusimamia na Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA) ni hatua mojawapo ya kuwakuza wazalishaji wadogo ili waweze kukua na hatimae kutoa mchango mkubwa katika nchi yetu kwa kuongeza ajira na uzalishaji. SMIDA imepewa majukumu ya kuwalea wazalishaji kwa kuwapatia mafunzo, sehemu ya kufanyia shughuli zao mpaka watakapoweza kusimama pamoja na kuwapatia ushauri wa kitaalamu. Ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya SMIDA, tayari Serikali imetoa eneo Maruhubi kwa ajili ya ujenzi wa Makao makuu na karakana na Kizimbani Pemba kwa ajili ya ofisi ndogo. Aidha, Wizara imepanga kuanzisha ofisi za SMIDA katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ili huduma zake ziweze kuwafikia wazalishaji wadogo walio wengi zaidi.

38. Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara inatarajia kuingia makubaliano ya mashirikiano na kampuni ya *'Linking African Markets and Partnership (LAMP)* ambayo itashirikiana na SMIDA kwa kutoa ushauri wa kitaalamu

katika masuala ya viwanda pamoja na kuzitangaza na kuziunganisha bidhaa zetu na masoko ya kitaifa, kikanda na kimataifa *(market linkage).* Aidha, LAMP itashirikiana na SMIDA katika kuandaa, kubainisha miradi ya wazalishaji wadogo na hatimae kusaidia kutafuta wadhamini wa miradi husika. Ni matumaini yetu kuwa mashirikiano haya yatapelekea SMIDA kusaidia wazalishaji kwa ufanisi na hatimae kuongeza uzalishaji pamoja na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi.

39. Mheshimiwa Spika, Katika kuhamasisha zaidi uwekezaji kwenye masuala ya viwanda, Wizara imepanga kuanzisha maeneo tengefu ya viwanda *(Industrial Parks)* kwa kila wilaya Unguja na Pemba. Katika awamu ya kwanza ya kutekeleza mpango huu, Wizara imepanga kuanzisha maeneo tengefu ya viwanda *(Industrial Parks)* katika maeneo matatu (3). Maeneo hayo yatakuwa ni chachu ya kuibua vipaji vya vijana na kuendeleza ubunifu katika masuala ya biashara, ujasiriamali, teknolojia na uzalishaji wa bidhaa kwa ujumla.

40. Mheshimiwa Spika, mbali ya kuhimiza wananchi wa ndani kuwekeza katika sekta ya viwanda, pia tunahamasisha wadau wa nje kuwekeza katika sekta hii. Wizara yangu inashirikiana na kampuni kutoka China ya *'Shanghai Ling Hang Group'* katika kutangaza fursa za Zanzibar ndani ya soko la China zikiwemo fursa za biashara, utalii na uwekezaji wa viwanda. Mnamo Aprili mwaka huu, Wizara yangu ilishiriki katika kongamano la biashara na uwekezaji lililofanyika China ambapo tulipata nafasi ya kukutana na wafanyabiashara na wawekezaji

mbali mbali ambao wameonesha nia ya kuja kuwekeza Zanzibar.

41. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mazingira bora ya biashara, hatua mbali mbali zinachukuliwa zikiwemo kuweka mfumo wa usajili biashara kwa njia ya kimtandao *(Online Registration System),* kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni zinazotawala sekta ya biashara na viwanda na kutekeleza mikakati na sera za biashara kwa kuendeleza uzalishaji na uongezaji wa thamani wa bidhaa za chumvi, dagaa, viungo, mafuta ya arki ya mimea na mwani kupitia uimarishaji wa makongano *(clusters)* na minyororo ya thamani *(value chains)* ya bidhaa hizo.

42. Mheshimiwa Spika, Serikali imekusudia kuyaendeleza maeneo ya mradi wa usarifu wa mazao ya kilimo yakiwemo matunda na mboga katika kiwanda kilichopo Pujini Pemba kilichojengwa kupitia mradi wa MIVARF na kituo cha kusarifu matunda Kizimbani Unguja kilichojengwa kwa msaada wa Korea ya Kusini. Maeneo haya yatageuzwa na kuwa maeneo tengefu ya kilimo - biashara *(Agri-business Parks).* Ili kuhakikisha uwepo wa bidhaa *(agricultural products)* za kutosha, Wizara imepanga kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pamoja na kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kilichopo Bambi na Mafunzo kinumoshi na langoni na halmashauri za Wilaya kwa ajili ya uzalishaji pamoja na kuhamasisha mabaraza ya vijana na wakulima kuzalisha mazao ya kilimo ambayo yatasarifiwa katika maeneo hayo tengefu.

43. Mheshimiwa Spika, kwa kuthamini umuhimu wa tafiti katika kutekeleza miradi na mipango yetu, Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na taasisi za utafiti ikiwemo Taasisi ya Utafiti wa Sera za Maendeleo 'Research and Poverty Alliviation (REPOA) na COSTECH. Hivi karibuni Wizara yangu ilishiriki katika warsha iliyoandaliwa na taasisi ya REPOA ya majadiliano ya kisera na utafiti juu ya umuhimu wa viwanda vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumudu ushindani *(Competitiveness)* katika kupata masoko ya bidhaa zetu ndani na nje ya nchi. Imeonekana kuwa bidhaa za viwanda vya Tanzania vikiwemo vya Zanzibar haziwezi kushindana vizuri na bidhaa za viwanda vya nje hivyo suala la kupanua nafasi katika mnyororo wa thamani linatakiwa kuhamasishwa ili viwanda vyetu viingie kwenye ushindani ndani ya masoko huria. Changamoto zinazokwamisha viwanda vyetu kufanya vizuri zikiwemo gharama za uzalishaji, ubora wa bidhaa, matumizi ya tafiti na teknolojia, matumizi mazuri ya fursa za masoko na kujua matakwa ya mtumiaji zitafutiwe suluhisho au ziondoshwe kabisa.

44. Mheshimiwa Spika, suala la Viwango ni jambo muhimu katika kuongeza ushindani *'Competitivenss'* wa bidhaa katika masoko ya ndani na nje. Ili bidhaa zetu zipate soko na zikubalike lazima zifikie ubora unaokubalika nchini na kimataifa. Ukamilishaji wa ujenzi wa maabara na ofisi za taasisi ya viwango umepangwa kufanyika ili kwenda sambamba na ukuaji wa mahitaji ya maabara unaotokana na ongezeko la ujenzi wa viwanda, uimarishaji wa bidhaa za wajasiriamali, ongezeko kubwa la uagizaji, uzalishaji, na matumizi ya gesi, mafuta na vifaa vya umeme ukiwemo

umeme unaotumia jua. Uimarishaji wa maabara ni hatua muhimu katika kujenga miundo mbinu ya viwango *(Quality Infrastructure)* ndani ya nchi ambayo itawezesha bidhaa zinazozalishwa nchini kukubalika katika masoko ya kimataifa. Ipo haja ya kuchukua maamuzi ya haraka ya kujenga na kuimarisha maabara na vituo vya kitaifa vya kutoa hati za ubora zikazotambulika.

45. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha zaidi sekta ya viwanda, Wizara yangu itaendelea kutia mkazo katika kuendeleza sekta ndogo za mwani, dagaa na chumvi. Kwa upande wa mwani ambao ni sekta ya pili ya kilimo inayochangia pato kubwa kwa nchi na pia imeajiri watu wengi wanawake, Wizara imepanga kusaidia kuanzishwa kwa kiwanda cha kusarifu zao la mwani ili kukabiliana na changamoto ya bei ndogo ya mwani. Usarifu huo utapelekea kutengenezwa kwa bidhaa maalum ya 'carrageneen' ambayo inaweza kuleta bei nzuri kwa kilo na hivyo kuinua kipato cha wakulima.

46. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa bidhaa ya *'carrageneen"* inapata soko ndani na nje ya nchi, Wizara yangu kwa kushirikiana na kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania *(COSTECH)* pamoja na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara ya Tanzania *(TANTRADE)* imepanga kufanya utafiti wa masoko *(market survey)* kwa bidhaa hiyo. Aidha, Mkakati wa kimasoko wa Tasnia ya Mali za Ubunifu na Utambulisho Maalum *'Intellectual Property and Branding'* utatumika kwa zao hili kwa ajili ya kulilinda na kuongeza thamani.

47. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bidhaa ya chumvi, Wizara yangu tayari imempata muwekezaji ambae atawekeza katika usarifu wa bidhaa hiyo ambapo kwa kuanzia ataunganishwa na wakulima wa shamba kubwa la chumvi la Ushirika la Shengejuu lililopo kisiwani Pemba. Wizara kwa upande wake itatoa usaidizi kwa wakulima wa chumvi katika kuweka miundo mbinu ya barabara pamoja na utayarishaji wa mabwawa ya kuvunia chumvi ili kuhakikisha kuwa uzalishaji wa chumvi unafanyika bila ya vikwazo vyovyote. Wizara itaendelea kuangalia maeneo mengine ya chumvi yaliyopo Pemba na Unguja ili nayo yafikie kiwango cha kimataifa.

48. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara inaendelea kusaidia viwanda vilivyopo kwa kupunguza changamoto za kukwama kuuza bidhaa zao Tanzania Bara ambapo Wizara yangu imeendelea kufanya vikao na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya Tanzania katika hatua za kutatua changamoto zinazokwamisha biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kimsingi, tumekubaliana kuondosha vikwazo vyote visivyo vya kiushuru (NTBs) na tumeweka utaratibu wa kutatua changamoto zinapotokea kwa kuwasiliana moja kwa moja *(Hotline)* na Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Nawahamasisha wenye viwanda Zanzibar na wawekezaji wote waendelee na shughuli zao za uzalishaji wakati juhudi za kutatua changamoto hizi zikiendelea kuchukuliwa.

49. Mheshimiwa Spika, Sekta binafsi ndiyo muhimili mkuu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, hivyo tunategemea

wataimarisha shughuli zao za uzalishaji bidhaa zenye viwango kwa mahitaji ya ndani pamoja na kuuza nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima (ZNCCIA) pamoja na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (ZIPA), na sekta nyengine katika kuboresha ujenzi wa uchumi wa viwanda. Ushirikiano huo upo katika ngazi zote kuanzia uandaaji wa Sera na hadi uhamasishaji wa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na ufuatiliaji na tathmini ya miradi inapoanzishwa.

50. Mheshimiwa Spika, Ili kuendelea kuhamasisha sekta binafsi, Baraza la Taifa la Biashara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na kampuni ya Magazeti ya Tanzania *(Tanzania Standards Newspapers – TSN)* limeandaa jukwaa la fursa za biashara na maendeleo za Zanzibar ambapo kupitia jukwaa hilo, Zanzibar iliweza kutangaza fursa zake zikiwemo fursa kwa viwanda vya kusarifu mazao ya baharini na kilimo. Jukwaa hili lilihudhuriwa na watu zaidi ya 300 wakiwemo mabalozi, wafanyabiashara, Serikali na watu binafsi kutoka ndani na nje ya nchi.

51. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Serikali, mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa katika mwaka wa 2017 umefikia asilimia 17.0 wakati Mchango wa sekta ndogo ya uzalishaji *(manufacturing)* umefikia asilimia 6.3 ambayo imepungua kutoka asilimia 6.9 kwa mwaka 2016. Kwa ujumla Sekta ya huduma inaendelea kuchangia kwa asilimia kubwa katika pato la Taifa kama

inavyoonekana katika mchoro Namb. 7 hapo chini. Hata hivyo dalili za kuimarika zaidi kwa sekta ya viwanda zinaendelea kujitokeza kutokana na mambo yafuatayo:

i. Kuimarika uzalishaji wa sukari katika kiwanda cha sukari, Mahonda, baada ya kukamilika ufungaji wa mitambo mipya na mikubwa zaidi ya kiwanda na utanuzi wa mashamba ya miwa pamoja na kuongezeka wakulima wa miwa wa nje *(outgrowers);*

ii. Kuanzishwa kwa Wakala wa Kusimamia na Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA);

iii. Kuimarika kwa uzalishaji na ubora wa bidhaa za viwanda vidogo vidogo na wajasiriamali wadogo wa sehemu mbalimbali za Unguja na Pemba. Miongoni mwa bidhaa hizo ni zile zinazotokana na mwani ambazo uzalishaji wake unatarajiwa kuongezeka kufuatia vikundi kumi na tano kupatiwa msaada wa vifaa vya usarifu wa mwani vilivyotolewa na UNIDO hivi karibuni;

iv. Kuimarisha usarifu wa chumvi inayozalishwa kisiwani Pemba; na

v. Kuendelea kwa hatua za kuanzisha kiwanda cha kusarifu samaki *(fish processing).*

Mchoro Namba 7: Mchango wa Sekta za Kiuchumi katika Pato la Taifa 2017.



4 UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MIPANGO YA WIZARA KWA MWAKA 2017 – 2018:

52. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi pamoja na mapitio ya hali ya biashara na viwanda, naomba sasa kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2017/2018.

Ukusanyaji wa Mapato

53. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu ilipangiwa lengo la kukusanya mapato ya **TZS 455.0 milioni** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2018, jumla ya **TZS. 864.34 milioni** zilikwishapatikana ikiwa ni makusanyo na kuingizwa katika Mfuko mkuu wa Serikali. Kiasi hicho

cha makusanyo ni sawa na asilimia 190 ya makisio ya makusanyo yote kwa mwaka wa fedha 2017 /2018.

54. Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa Mapato hayo ni kama unavyoonekana katika Jadweli Nam.4 hapa chini;

Jadweli Nam 4:
Mapato ya Wizara kwa Kipindi cha Julai 2017 – Machi 2018 (Tzs. Mil)

KIFUNGU	MAELEZO	Makadirio Julai– Machi	Makusanyo Julai– Machi	Asilimia ya Makusanyo Julai - Machi
R1146	**Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko**	**160.00**	**310.92**	**194**
1422014	Ukaguzi wa Mezani na Vipimo	95.00	28.20	29.68
1422077	Malipo ya Kazi za Biashara	65.00	282.72	434.95
R0106	**Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali**	**294.00**	**276.15**	**93.92**
1146002	Ada ya Mali Maiti	1.00	0.58	58
1422030	Alama za Biashara	156.00	65.36	41.90
1422031	Uandikishaji wa Makampuni	81.00	119.53	147.57
1422032	Uandikishaji wa Majina ya Biashara	31.00	34.41	111
1422034	Ujira wa Kutengeneza Nyaraka	26.00	156.27	602.69
	Mapato Mengineyo		177.26	**-**
	Mapato Mengineyo ZRB(18)		149.11	
	Mapato Mengineyo STAMP		28.15	
Jumla Kuu		**455.00**	**864.34**	**189.96**

Chanzo: Wizara ya Biashara na Viwanda, 2018

55. Mheshimiwa Spika, makusanyo hayo makubwa yanatokana na idadi kubwa ya wananchi kusajili nyaraka za kubadilisha umiliki wa vyombo vya moto kufuatia zoezi lililofanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) la kuwataka wananchi wanaomiliki vyombo vya moto kuhakikisha kadi za vyombo hivyo zina majina ya wamiliki halisi wa vyombo hivyo. Aidha, ongezeko hilo linatokana na kutumika kwa sheria mpya ya kampuni ambayo pamoja na kuboresha masharti pia imeweka utaratibu mzuri zaidi wa ada mbalimbali ambao umesaidia kuongezeka kwa utii wa sheria *(compliance)* kwa kampuni nyingi.

Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018

56. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa matumizi, Wizara ilitengewa jumla ya **TZS 7,210.20 milioni** kwa ajili ya kutekeleza program zake kwa mwaka 2017- 2018. Hadi kufikia Machi 2018, Wizara iliingiziwa jumla ya **TZS 4,080.91 milioni** ambazo ni sawa na asilimia 56.60% ya bajeti ya mwaka. Mchanganuo wa matumizi hayo kwa kila program ulikuwa kama unavyoonekana katika Jadweli Nam. 5.

Jadweli Namba 5
Matumizi ya Fedha kwa kipindi cha Julai 2017 – Machi 2018

WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA					
S/N	**Programu Kuu**	**Fedha Zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Tzs**	**Fedha Zilizopatikana kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai - Machi, 2018) Tzs**		**Asilimia ya Fedha Iliyopatikana**
PRO1	**Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara**	**2,344,357,876**	**1,798,441,831**		76.71%
	Utawala na Uendeshaji wa Wizara	1,613,131,274	1,262,442,401		78.26%
	Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti	340,914,830	188,535,957		55.30%
	Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba	390,311,772	347,463,473		89.02%
PR02	**Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali**	**912,580,734**	**305,969,943**		33.53%
	Ukuzaji Viwanda	644,986,732	271,563,622		42.10%
	Maendeleo ya Ujasiriamali	267,594,002	34,406,321		12.86%
PR03	**Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara**	**1,469,461,390**	**1,109,791,454**		75.52%
	Ukuzaji Masoko na Usafirishaji	316,203,715	244,222,910		77.24%
	Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji	143,336,319	81,027,559		56.53%
	Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji biashara za ndani	502,200,000	364,308,000		72.54%
	Usajili wa Biashara na Mali	507,721,356	420,232,985		82.77%
PR04	**Viwango na Tathmini ya Ubora.**	**2,483,800,000**	**866,705,955.25**		34.89%
	Viwango na Udhibiti Ubora.	2,483,800,000	866,705,955.25		34.89%
	JUMLA KUU	**7,210,200,000**	**4,080,909,183**		56.60%

Chanzo: Wizara ya Biashara na Viwanda, 2018

Utekelezaji wa Malengo ya Wizara

57. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Biashara na Viwanda ulifanyika kulingana na huduma na shughuli zilizowekwa katika programu za Wizara kama ifuatavyo:

4.1 PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

58. Mheshimiwa Spika, Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda imeundwa na Programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji wa Wizara; Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti; na Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba. Katika kutekeleza majukumu yake, program hii ilipangiwa matumizi ya **TZS 2,344.36 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, hadi kufikia Machi 2018, programu hii imeingiziwa jumla ya **TZS 1,798.44 milioni** ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na asilimia 76.71 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

4.1.1 Programu ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara:

59. Mheshimiwa Spika, Programu hii ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Kwa mwaka wa fedha 2017

– 2018, programu hii ndogo ilikuwa na jukumu la kutoa huduma ya ununuzi wa vifaa vya ofisi na usafiri pamoja na huduma ya usimamizi wa rasiliamli watu na huduma kwa ujumla ambayo inahusisha kazi za uimarishaji wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi, utoaji wa huduma kwa Idara zote za Wizara na uratibu wa mikutano ya majadiliano ya ndani, ya kikanda na ya kimataifa. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya **TZS 1,613.13 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018.

Hadi kufikia Machi 2018, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **TZS 1,262.44 milioni** ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na asilimia 78.26 ya makadirio ya mwaka. Huduma za Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji zilitekelezwa kama ifuatavyo:-

Usimamizi wa Rasilimali Watu na Huduma kwa Ujumla:

60. Mheshimiwa Spika, Kwa madhumuni ya uimarishaji wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi, Wizara imeendelea kuwalipa wafanyakazi wake mishahara yao na Stahiki zao kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Wizara iliwapatia wafanyakazi wake likizo zao na stahiki za likizo hizo. Kadhalika, Wizara imeimarisha mazingira ya kufanyia kazi na kuimarisha usalama. Ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu yetu, Wizara imefanya Uajiri wa wafanyakazi wanne wapya. Aidha, jumla ya nafasi kumi na moja (11) zimeshatangazwa na Tume ya Utumishi Serikalini.

61. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu na kuwapatia mafunzo watumishi wake kulingana na Mahitaji husika ambapo jumla ya wafanyakazi nane (8) wanaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Sheria, Uongozi wa Biashara, Uchumi, Uhandisi, Manunuzi na Ugavi. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya Wafanyakazi nane (8) wamerudi kutoka masomoni katika fani ya Sheria, Biashara, Uchumi, Uhasibu na Manunuzi na Ugavi.

62. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utoaji wa huduma, jumla ya wafanyakazi saba (7) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kati ya hao watumishi watatu (3) wamepatiwa mafunzo elekezi ya awali *(Induction Course)* ili kuwajengea ufahamu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maadili ya Kazi katika utumishi wa umma kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi, watumishi wawili (2) wamepatiwa mafunzo ya Uandishi wa Sheria *(legislative Drafting),* mfanyakazi mmoja Uhifadhi na Usalama wa Taarifa za Wizara na mfanyakazi mmoja (1) amepatiwa mafunzo ya Utawala na Uongozi *(Leadership and Management).*

63. Mheshimiwa Spika, Katika kuendeleza ushiriki wa viongozi wa Wizara katika Mikutano ya sekta ya Biashara na Viwanda nchini, Kikanda na Kimataifa, Wizara ilishiriki Mikutano ya majadiliano ya biashara katika ngazi za wataalamu na Mawaziri. Mikutano hiyo ya majadiliano ilifanyika katika kanda za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya SADC na WTO. Aidha, Wizara yangu kwa ilishiriki vikao mbali mbali vikiwemo vya Zanzibar – China

Forum kilichofanyika China, Mkutano wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mkataba wa EAC, Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo ya kusini mwa Afrika SADC uliofanyika katika mji wa Pretoria nchini Afrika Kusini,Mkutano wa WTO uliofanyika *Buenos Aires - Argentina* na Mkutano kwa ajili ya kuhudhuria Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika AFCFTA pamoja na mkutano wa kamati ya Fedha na Uchumi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na India.

Huduma ya Ununuzi wa Vifaa vya Ofisi

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia mpango wake wa manunuzi *(annual procurement plan)* na kwa lengo la kusimamia vyema matumizi ya fedha za umma kwa mujibu wa sheria ya manunuzi, Wizara ilifanya manunuzi ya vifaa vya kuandikia, mafuta, Vespa, kompyuta, samani na vifaa vya usafi, huduma za umeme, maji na simu. Vifaa vyote hivi na huduma vimepatikana kwa wakati. Aidha, Wizara ilinunua Magazebo ambayo yaliwasili mwezi Januari na yaliwezesha kufanyika kwa Tamasha la nne la biashara la Zanzibar kwa ufanisi.

4.1.2 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

65. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti ilikuwa na jukumu la kutayarisha, kuchambua na kutathmini utekelezaji wa mipango na malengo maalum ya Wizara. Huduma ambazo zimesimamiwa na Programu hii ndogo ni Uandaaji na

Uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara, Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Wizara na Usimamizi wa Takwimu za Biashara. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya **TZS 340.91 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018.

Hadi kufikia Machi 2018, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **TZS 188.53 milioni** ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na asilimia 55.30 ya makadirio ya mwaka.

66. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara, huduma ambazo nimezitaja hapo juu zimetekelezwa kama ifuatavyo: -

Uandaaji na Uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara

67. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza huduma hii, Wizara inaendelea na matayarisho ya kuandaa Sera za Biashara na Viwanda ili kurahisisha uwekezaji na biashara Zanzibar. Katika kufanikisha kazi hii, tayari Wizara kwa kushirikiana na *'Trade Mark East Africa'* imeshampata mshauri elekezi wa kuandaa Sera ya Biashara ambayo itazingatia makubaliano katika ngazi za kikanda na kimataifa. Aidha, katika kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji kwa sekta binafsi, Wizara yangu kwa kushirikiana na mshauri elekezi kutoka taasisi ya *'Economic and Social Research Foundation' (ESRF)* inatayarisha Sera ya Maendeleo ya sekta binafsi ambapo rasimu ya awali ya Sera hiyo imewasilishwa Wizarani kwa ajili ya kupata maoni katika ngazi ya Wizara na wadau husika kutoka Serikali na sekta binafsi.

68. Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuendeleza viwanda hapa nchini, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(United Nation Industrial Development Organization – UNIDO)* imeshatayarisha rasimu ya sera ya viwanda ambayo inatilia mkazo maeneo makuu manne (4) ambayo ni uzalishaji, kuongeza thamani na viwango (manufacturing, value addition and quality standards), uzalishaji na muunganiko wa kisekta *(manufacturing and sector linkages)*, masuala ya bahari (blue economy –fishing and aquaculture) na maendeleo ya utalii, kodi na masuala ya usimamizi *(tourism development, rent allocation and management)*. Ni imani ya Wizara yangu kwamba utekelezaji wa miradi katika maeneo hayo yatakuwa ni chachu ya maendeleo ya viwanda hapa Zanzibar pamoja na kutoa ajira kwa vijana wetu. Wizara itatoa vijalada *(fliers)* kuwawezesha wadau kuelewa taratibu za kikanuni na sheria kwa bidhaa na usafirishaji wake kwa kuzingatia ubora.

69. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya *(European Union – EU)* kupitia mradi wa TradeCom II imefanya utafiti wa thamani katika viungo, mwani na mboga mboga *(Value Chain Analysis on Agro Processing Industries for Spices, Seaweeds and Horticulture)* kwa ajili ya kubainisha changamoto za kiushindani zinazokabili mazao hayo katika masoko ya kimataifa. Utafiti huo umepelekea kuandaliwa kwa muongozo wa kuimarisha ubora *(Guide to manage Product Quality in the Zanzibar Pemba Export Corridor: Recommendations for Quality Management Improvement)* ambao umewasilishwa kwa wadau kwa upande wa Zanzibar na Tanzania bara kwa

kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Sera za Maendeleo *(Research and Poverty Alliviation – REPOA).* Aidha, kutokana na utafiti huo, taarifa fupi za sera *(policy briefs)* juu ya masuala ya mwani na viungo zimetayarishwa ili zisaidie kutoa muongozo katika maandalizi ya mipango na sera za nchi yetu.

70. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa tunapunguza vikwazo vya biashara ndani ya Zanzibar na baina ya Zanzibar na Tanzania bara, Wizara kwa kushirikiana na *TradeMark East Africa (TMEA)* inafanya utafiti wa utambuzi wa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru *(Non Tarrif Barriers –NTBs)* ambapo tayari mshauri elekezi ameanza kufanya kazi hiyo na kutayarisha rasimu ya ripoti ya awali *(Inception Report).* Wizara inategemea kuwa matokeo ya utafiti huo yatasaidia kuweka mikakati madhubuti zaidi ya kuimarisha biashara baina ya pande hizi mbili za nchi.

Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Wizara

71. Mheshimiwa Spika, Kazi za kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kazi za kawaida zinaendelea kufanyika kwa kushirikiana na Tume ya Mipango ambapo ripoti za utekelezaji wa miradi na kazi za kawaida kwa kila kipindi cha robo mwaka zinaandaliwa. Aidha, katika kufanya matayarisho ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara imeandaa vipaumbele kwa sekta ya Biashara na Viwanda. Vipaumbele hivyo ni Kuendeleza viwanda kwa kuimarisha na kuongeza thamani bidhaa za viungo, chumvi na mwani, Kuimarisha mazingira

bora ya biashara, Utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa Kusimamia na Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati *(Small and Medium Industry Development Agency - SMIDA)* na Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Majengo na maabara ya Taasisi ya Viwango Maruhubi.

72. Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya kitaifa, Wizara yangu inakondoesha masuala mtambuka katika shughuli zake yakiwemo masuala ya mazingira, ulemavu, UKIMWI na jinsia. Katika mwaka wa fedha 2017-2018, Wizara ilifanya warsha kwa wafanyakazi hasa wa ngazi za chini wakiwemo madereva, matarishi, makarani na walinzi juu ya umuhimu wa kukondoesha na kuzingatia masuala mtambuka katika utendaji wa kazi zao. Mafunzo hayo yalifanikiwa kwa wafanyakazi kuhudhuria kikamilifu na kushiriki katika majadiliano.

Usimamizi wa Takwimu za Biashara

73. Mheshimiwa Spika, Wizara imeona udhaifu katika kupata takwimu za biashara na viwanda hivyo imefanya kikao pamoja na wafanyabiashara cha kujadili umuhimu wa taarifa za biashara na viwanda ili kuhakikisha kuwa inaimarisha takwimu inazozikusanya. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imetoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya masuala ya takwimu pamoja na kujadili njia bora za ukusanyaji wa Takwimu za Wizara. Vikao hivyo pamoja na mafunzo vimelenga kukabiliana na changamoto za ukusanyaji wa takwimu ambazo ni pamoja na takwimu kurikodiwa katika vipimo visivyokuwa rasmi (korja, gunia), kurikodiwa kwa takwimu

zisizo sahihi, kutumika kwa njia tofauti za ukusanyaji wa takwimu n.k.

74. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa tunasimamia vizuri taarifa za takwimu, Wizara imepanga kuanzisha mfumo wa taarifa za takwimu *(Trade Management Information System)* ambapo tayari dhana ya mradi wa mfumo huo wa taarifa imeandaliwa na kuwasilishwa kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo *(United Nations - Food and Agriculture Organisation –FAO)* kwa ajili ya udhamini. Mradi wa mfumo takwimu za biashara utahusisha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi, kutengeneza mfumo wa takwimu za biashara na viwanda pamoja na kuandaa mpango mkakati *(Strategic Plan)* wa takwimu.

4.1.3 Programu ndogo ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

75. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kutekeleza na kusimamia shughuli zote za Wizara ya Biashara na Viwanda kwa upande wa kisiwa cha Pemba. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya **TZS 390.31 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018, na hadi kufikia Machi 2018, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **TZS 347.46 milioni** ikiwa ni mishahara na kazi nyengine za kawaida sawa na asilimia 89.02 ya makadirio ya mwaka. Huduma iliyopangwa kutolewa na Programu hii imetekelezwa kama ifuatavyo:-

Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

76. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza huduma hii, Wizara ilifanya shughuli mbali mbali zikiwemo;

i. Utoaji wa huduma na ununuzi wa vifaa ambapo Wizara kupitia Afisi Kuu Pemba ilifanya ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi, ununuzi wa huduma za umeme, maji na mawasiliano, kufanya matengenezo ya magari, ununuzi wa mafuta na kutoa huduma ya usafiri kwa maafisa wa wizara kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi mbali mbali za wizara;

ii. Uimarishaji wa mazingira ya Kazi ambapo jumla ya wafanyakazi wanne (4) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi yanayohusiana na masuala ya biashara na utawala. Aidha Wizara kupitia ofisi kuu Pemba iliwapatia wafanyakazi kumi na mbili (12) likizo pamoja na kuwapatia malipo yao stahiki;

iii. Kufanya ukaguzi wa vikundi 48 vya wajasiriamali katika Wilaya zote za Pemba na kuwasaidia katika shughuli zao za uzalishaji pamoja na kuwasaidia baadhi ya gharama za kushiriki katika maonesho mbali mbali ya kibiashara kama vile Sabasaba, Tamasha la Biashara la Zanzibar na Tamasha la Juakali Burundi;

iv. Kufanya ukaguzi wa mizani na vipimo kwa mujibu wa Sheria ya Mezani na Vipimo Nam 1 ya mwaka 2004 ambapo jumla ya mizani 670, mita ndogo za mafuta 13, mita 3 kubwa za kutolea mafuta katika bandari ya

Wesha, magari 11 ya kubebea mafuta zimekaguliwa katika shehia mbali mbali za wilaya zote za Pemba na

v. Kufanya ukaguzi wa maduka, maghala na bekari kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani halali wa kibiashara na kumlinda Mtumiaji Nam 2 ya mwaka 1995. Katika ukaguzi huo jumla ya maduka 1152 maghala 34 na bekari 37 zimekaguliwa. Kaguzi zote hizi hufanyika ikiwa ni sehemu za hatua za kuwalinda watumiaji kwa kuhakikisha ubora na usalama wa bidhaa zinazouzwa.

4.2 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

77. Mheshimiwa Spika, Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda ambayo utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inajumuisha Programu ndogo mbili ambazo ni Ukuzaji Viwanda na Maendeleo ya Wajasiriamali. Program hii kuu ilipangiwa jumla ya **TZS 912.58 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018. Hadi kufikia Machi 2018, programu hii kuu imeingiziwa jumla ya **TZS 305.97 milioni** ikiwemo mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida, sawa na asilimia 33.53 ya makadirio ya mwaka. Program ndogo hizo utekelezaji wake ni kama ufuatavyo:-

4.2.1 Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda

78. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda ina jukumu la kutoa huduma za kuimarisha sekta

ya viwanda na kutoa msaada kwa wajasiriamali. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **TZS 644,98 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018, na hadi kufikia Machi 2018, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **TZS 271.56 milioni** ikiwemo mishahara na kazi nyengine za kawaida, sawa na asilimia 42.10 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa program ndogo ya Ukuzaji Viwanda ulikuwa kama ifuatavyo:-

Uimarishaji wa Sekta ya Viwanda

79. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza huduma hii, Wizara kwa kushirikiana na UNIDO inaendelea na kazi ya kuandaa Sera ya Viwanda ambapo tayari rasimu ya awali imeshajadiliwa na wadau katika ngazi ya Wizara na taasisi zilizo chini yake. Sera hiyo inategemewa kutoa muongozo wa kuendeleza sekta ya viwanda hapa nchini. Sera hiyo itahusisha pia utengenezaji wa mkakati wa maendeleo ya viwanda. Hatua inayofuata sasa ni kuipeleka serikalini kwa kukubaliwa na kuendelea na hatua zinazofuata.

80. Mheshimiwa Spika, ili kukuza uzalishaji wa chumvi hasa katika Jumuiya ya Chumvi ya AZASPO iliyopo kisiwani Pemba, Wizara yangu imesaidia kuleta mabadiliko ya kiutendaji ya jumuiya hiyo ili iweze kujiendesha kibiashara na hatimae kutoa mchango mzuri katika uchumi. AZASPO imebadilishwa kutoka hali ya 'Jumuiya' na kuwa 'Ushirika' ambapo pia uongozi mpya umechaguliwa kwa ajili ya kuimarisha zaidi utendaji. Wakati mabadiliko haya yanatokea, wanachama na wananchi kwa ujumla walihamasishwa juu ya umuhimu wa mabadiliko hayo

ili kurahisisha utekelezaji wake. Kwa sasa ushirika wa AZASPO upo katika hatua ya kuandaa Mpango wa Biashara *(Business Plan)* kwa ajili ya kuwa muongozo pamoja na kusaidia katika kuomba ufadhili kutoka mashirika na taasisi mbali mbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara imegharamia ujenzi wa kipande cha njia (barabara ya kifusi yenye makalavati) yenye urefu wa mita 300 katika eneo la Ambasha, Pemba kwa lengo la kurahisisha usafirishaji wa chumvi kutoka mashamba yaliyo sehemu hiyo.

81. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Kusimamia na Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati *(Small and Medium Industry Development Agency – SMIDA* ina wajibu wa kuchochea ukuaji wa viwanda hapa nchini kwa kukuza uwezo wa wazalishaji wadogo na wa kati katika kutengeneza na kuzalisha bidhaa zenye viwango vizuri. Ili kuimarisha SMIDA, sheria yake imeshapitishwa na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo Januari 2018 na tayari Mkurugenzi Mkuu na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wameshateuliwa mnamo Februari, 2018. Wakala inajipanga kuwa na eneo la kazi, kusimamia sera ya wajasiriamali, viwanda na mipango itakayojiwekea ya muda mfupi na muda mrefu kwa kuanzia na mradi wa maendeleo kila wilaya kwa kuzingatia rasilimali zilizopo na nyenzo zilizopo za kila wilaya.

82. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa zao la mwani katika uchumi pamoja na ajira kwa wananchi hasa wanawake, Wizara yangu kwa kushirikiana na UNIDO imetoa msaada kwa kongano la mwani *(Zanzibar*

Seaweed Cluster Initiative) ambalo linakusanya vikundi 14 vyenye wajumbe zaidi ya 300 kutoka Unguja na Pemba. Msaada huo umehusisha vifaa vya kusarifu mwani kama 'blenders', 'extruders', meza na chupa za kuhifadhia bidhaa zinazotokana na mwani. Wawakilishi wa vikundi vilivyopatiwa msaada wa vifaa wamepatiwa mafunzo ya matumizi bora na utunzaji wa vifaa vinavyohusika. Vile vile katika msaada huo zimo boti ndogo *(barges)* zinazotumika katika uvunaji wa mwani. Hii ni hatua moja wapo ya kuongeza thamani ya zao la mwani.

83. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuhusiana na sekta ndogo ya chumvi, Wizara imepata muwekezaji ambae amepanga kuanzisha kiwanda cha kusarifu chumvi na kuiuza ndani na nje ya nchi hasa katika soko la Ulaya. Muwekezaji huyo alipata fursa za kutembelea mashamba ya chumvi yaliyopo kisiwani Pemba ambapo kiasi cha kilo 250 ya chumvi ilikusanywa kwa ajili ya kufanyiwa utafiti. ili kuhakikisha kuwa chumvi inayozalishwa ina viwango bora, muwekezaji huyo ameazimia kutafuta wataalamu kutoka Bagamoyo ili kuwapatia mafunzo wazalishaji wa chumvi. Kwa sasa Wizara yangu inatarajia kuweka mpango bora wa kusimamia bidhaa hiyo ili kuleta maendeleo katika sekta hiyo ndogo.

4.2.2 Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali

84. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ina jukumu la kutoa msaada wajasiriamali. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya TZS 267.59 milioni

kwa mwaka wa fedha 2017 – 2018. Hadi kufikia Machi 2018, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya TZS 34.41 milioni kwa kazi za kawaida, sawa na asilimia 12.86 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa program ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ulikuwa kama ifuatavyo:-

Kutoa Msaada kwa Wajasiriamali

85. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwaendeleza wajasiriamali, Wizara imefanya vikao viwili (2) vya kamati ya ushauri ya wajasiriamali ambayo inaundwa na wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta ya Serikali. Kupitia vikao hivyo wajumbe wanajadiliana juu ya kazi za wajasiriamali, changamoto wanazokumbana nazo pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu ili kutoa suluhisho kwa changamoto zilizopo. Licha ya vikao, Wizara pia ilifanya ukaguzi wa miradi midogo midogo ya Viwanda pamoja na wajasiriamali kwa lengo la kutathmini maendeleo yao pamoja na kuwapatia ushauri wa kitaalamu. Wizara inakamilisha mapitio ya sera ya wajasiriamali ya mwaka 2006 na itawasilishwa Serikalini itakapokamilika.

86. **Mheshimiwa Spika,** mkazo zaidi umewekwa katika sekta ambazo zenye faida na uwezo wa kutoa ajira kwa wingi. Wizara yangu kupitia mradi pacha wa biashara na utalii wa kushajihisha viwanda kwa sekta ya utalii imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 30 ya ushoni na mitindo kwa viwango vya kimataifa ili kupata masoko ya utalii na ya kimataifa. Mafunzo hayo yatapelekea kupata utambulisho wa bidhaa *(Zanzibar Signature Product)* za ushoni na mitindo ya Zanzibar. Aidha, Wizara imezindua mradi wa 'Made in

Zanzibar' ambao unabeba miradi midogo ikiwemo Afya na Maisha Bora '*Wellness and Health Industry',* uzalishaji *'Manufacturing'* na uongezaji wa thamani *'Value Addition'*. Lengo la miradi yote hii ni kulitumia vizuri jina la Zanzibar ambalo tayari lina sifa nzuri ulimwenguni ili kuzitangaza bidhaa za Zanzibar katika masoko ya ndani na nje mkazo ukiwa matumizi ya bidhaa hai *(organic products)* kuwa ni muelekeo wa siku za mbele katika uchumi wa kusarifu kilimo.

87. Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo mafanikio kwa baadhi ya viwanda ikiwemo cha sukari, bado kuna changamoto zinazozikabili viwanda vilivyopo nchini. Wizara itaendelea kuzifuatilia changamoto hizo na kuzipatia ufumbuzi. Kwa upande wa kiwanda cha Sukari, changamoto itakayobakia ni kupatiwa maeneo ya kulima miwa hivyo Serikali inaendelea kuwatafutia maeneo hayo pamoja na kuwashajihisha wakulima waendelee kulima miwa ili kiwanda kiweze kuzalisha sukari kwa mashine zake za kisasa ambazo zina uwezo wa kusindika miwa ya kutosheleza matumizi.

Kwa upande wa kiwanda cha COTEX, Wizara tayari imezungumza na muwekezaji wa kiwanda hicho ili kutafuta njia mbadala ya kukitumia au kukiendeleza.

4.3 PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

88. Mheshimiwa Spika, Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara inajumuisha Programu ndogo nne (4) ambazo ni Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji, Ushindani

Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji, Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani pamoja na Usajili wa Biashara na Mali. Program hii ilipangiwa matumizi ya **TZS 1,469.46 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018.

Hadi kufikia Machi 2018, programu hii imeingiziwa jumla ya **TZS 1,109.79 milioni** ikiwemo Mishahara, Ruzuku, Miradi na kazi nyengine za uendeshaji, sawa na asilimia 75.52 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

4.3.1 Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji

89. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Biashara na Masoko pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Huduma ambazo zimesimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni uimarishaji wa mazingira mazuri ya biashara pamoja na kuongeza Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara.

Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **TZS 316.20 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018. Hadi kufikia Machi 2018, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **TZS 244.22 milioni** kwa ajili ya mishahara na kazi nyengine za kawaida sawa na asilimia 77.24 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma za program ndogo hii ni kama ifuatavyo;

Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara

90. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kufanya mapitio ya hali ya masoko kwa bidhaa zetu na kuangalia changamoto zilizopo. Shughuli mbali mbali za kupanua masoko ya bidhaa za Zanzibar na fursa zilizopo zilipitiwa ili tuweze kuingia katika masoko ya kanda ikiwemo Afrika ya Mashariki, SADC pamoja na nchi za Mashariki ya mbali, nchi za Ghuba ikiwemo UAE, Oman, Kuwait, Iran, nk.

Aidha, Wizara iliratibu ushiriki wa Zanzibar katika Maonesho ya 41 ya Kimataifa ya Biashara (Saba Saba) yaliyofanyika huko Dar es salaam mwezi wa Julai 2017. Taasisi zilizoshiriki ni pamoja na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC), Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi ya Zanzibar (ZIPA) na wajasiriamali wengine kutoka Unguja na Pemba. Bidhaa ambazo zilionyeshwa na wajasiriamali walioshiriki katika maonesho hayo ni pamoja na bidhaa za kusindika, kazi za mikono, dawa za asili, sabuni, bidhaa za viungo na nyenginezo.

91. Mheshimiwa Spika, kupitia maonesho hayo, wajasiriamali wetu wanapata fursa za kutangaza bidhaa zao na hivyo kupata wateja zaidi. Aidha, wajasiriamali wanapata fursa ya kujifunza kutoka kwa wenzao pamoja na kubadilishana mawazo na kujenga mahusiano *(business network)* kwa ajili ya kushirikiana katika biashara zao.

92. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushiriki wa maonesho ya Kikanda ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Wizara yangu iliratibu ushiriki wa wajasiriamali kutoka

Zanzibar katika Maonesho ya Jua Kali/Nguvu kazi yaliyofanyika Bujumbura nchini Burundi ambapo jumla ya wajasiriamali 12 walishiriki katika maonesho hayo. Katika kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanatumia fursa ya maonesho hayo ipasavyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mpango wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) iliwalipia wajasiriamali hao gharama za ushiriki katika maonesho hayo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango pamoja na MKURABITA imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 100 katika Mkoa wa Kaskazini A kwa upande wa Unguja na Micheweni Pemba. Mafunzo hayo yamelenga kuwashajihisha wajasiriamali kurasimisha biashara zao kwa kujisajili ili kuweza kupata fursa zinazopatikana katika biashara ya mfumo rasmi.

93. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia iliratibu ushiriki wa Zanzibar katika maonesho ya biashara yaliyofanyika jijini Nairobi nchini Kenya ikiwa ni maadhimisho ya siku ya Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wajasiriamali 3 hasa wanaohusiska na usarifu wa bidhaa za viungo *(spices)* walipata nafasi ya kutangaza bidhaa zao na hivyo kupanua masoko pamoja na wajasiriamali hao, pia walishiriki ZSTC na Kamisheni ya Utalii.

94. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuandaa utaratibu wa kuwa na ratiba ya matamasha na maonesho ya kibiashara ili iwawezeshe wajasiriamali kupata fursa za kutangaza na kuuza bidhaa zao. Wizara imeanza kukusanya taarifa za kuandaa ratiba ya matamasha na maonesho ya kibiashara nchini kutoka kwa wadau husika wakiwemo Wizara ya Kazi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii,

Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU). Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kupata maeneo ya kudumu ya kufanyia matamasha na maonesho ya kibiashara likiwemo eneo la Kilimani.

95. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyengine ambayo imechukuliwa ya kuhakikisha wajasiriamali wanaweza kupata masoko ya bidhaa zao, Wizara ilitayarisha Tamasha la Biashara ambalo hufanyika kila mwaka kama ni sehemu ya kuadhimisha Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka huu, Wizara iliandaa Tamasha la nne (4) la Biashara ambalo lilijumuisha jumla ya washiriki 219 wakiwemo washiriki watatu (3) wa kigeni mmoja kutoka Misri na wawili kutoka Kenya.

96. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuchangamsha Tamasha hilo la Biashara, Wizara iliaandaa majadiliano katika siku maalum *(special days)* tano (5) ambazo ni siku ya mwani *(Seaweed Day),* Siku ya Viwanda (Industrial Day), Siku ya Utalii *(Tourism Day),* Siku ya Bidhaa za Zanzibar *(Made in Zanzibar Day)* na Siku ya Afya *(Wellness Day).*

Lengo kuu la kuweka majadiliano hayo katika siku hizo maalum ni kuwakutanisha watumiaji na wazalishaji wa bidhaa hizo pamoja na kujua changamoto za sekta hizo. Aidha, majadiliano hayo yamesaidia kuweka wazi zaidi matumizi ya bidhaa husika.

Uimarishaji wa Mazingira Mazuri ya Biashara

97. Mheshimiwa Spika, Katika bajeti iliyopita nilieleza kuwa awamu ya mwanzo ya mkakati wa utambulisho maalum 'Branding' wa Karafuu ilikwisha zinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein mnamo mwezi wa Januari, 2017. Napenda kuliarifu Baraza lako kwamba Wizara yangu inaingia katika awamu ya pili ya utekelezaji wa shughuli za mkakati wa 'Branding' ya Karafuu ya Zanzibar kwa mwaka ujao wa fedha wa 2018/2019.

98. Mheshimiwa Spika, mbali ya kuwepo kwa mkakati wa *'Branding' ya karafuu,* mradi wa kukuza jina la Zanzibar *(Made in Zanzibar Project)* umeanzishwa ambao utekelezaji wake utatoa faida kwa sekta tofauti 'multiplier effects' zikiwemo sekta ya kilimo, biashara na utalii. Mradi huu katika awamu ya kwanza utahusisha utafiti katika sekta ndogo ya nguo *(textile and garment sector),* viungo *(spices),* afya *(wellness)* na mapishi (culinary) ili hatimae kuja na Mpango wa Biashara *(Business Plan)* ambao pamoja na mambo mengine mpango huo utaainisha malengo ya mradi na mikakati ya kufikia malengo hayo.

99. Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa kujenga uwezo wa kukondoesha Biashara *(Trademainstreaming Program),* Wizara yangu imewapatia wafanyakazi mafunzo juu ya usalama wa taarifa *(data security)* ili kujenga uelewa juu ya umuhimu wa kutunza taarifa za Serikali. Mafunzo hayo yaliwahusisha wafanyakazi wa Wizara kutoka idara na taasisi zake pamoja na taasisi nyenginezo za Serikali.

Mafunzo hayo yamejenga uelewa kwa washiriki juu ya kutunza taarifa na kuzilinda ili zisije zikatumiwa katika njia zisizostahiki.

100. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha matamasha na maenesho ya Biashara hapa Zanzibar, Wizara ilinunua magazebo na vifaa vyengine kwa ajili ya uandaaji wa matamasha na maonesho hayo. Ununuzi huo pia umesaidia kupungua kwa gharama za uendeshaji wa matamasha na maenesho hayo ambapo hapo awali Wizara yangu ililazimika kukodi magazebo hayo kutoka Tantrade. Magazebo na vifaa hivyo vilianza kutumika katika Tamasha la nne (4) la Biashara lililofanyika mwaka huu.

4.3.2 Programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji

101. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji inasimamiwa na Kitengo cha Mizani na Vipimo, Tume ya Ushindani Halali wa Biashara pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Huduma ambayo imesimamiwa na kutekelezwa na program ndogo hii ni huduma ya kuimarisha ushindani halali wa kibiashara. Program ndogo hii ilipangiwa jumla ya **TZS 143.34 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018. Hadi kufikia Machi 2018, programu hii imeingiziwa jumla ya **TZS 81.02 milioni** kwa ajili ya mishahara na kazi nyengine za kawaida sawa na asilimia 56.53 ya makadirio ya mwaka huduma za programu hii ndogo ilitekelezwa kama ifuatavyo:

Uimarishaji Ushindani Halali wa Kibiashara

102. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya Tume, Sheria ya Tume ya Ushindani Halali wa Biashara imeshapitishwa na Baraza la Wawakilishi na uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa tume hiyo umeshafanyika. Kazi kuu za Tume hiyo kwa mujibu wa sheria ni zifuatazo;

i. Kusimamia masuala ya ushindani halali wa biashara baina ya wafanyabiashara na makampuni.

ii. Kuzuia mienendo ya biashara isiofaa kama vile matumizi mabaya ya nguvu za soko, kupandisha bei ili kumuondosha mpinzani na vitendo vya kuwaengeua washindani.

iii. Kusimamia maeneo mahsusi ya kumlinda mtumiaji yakiwemo kutambulisha bei za bidhaa na huduma (price dispalay), dhamana kwa bidhaa *(product guarantee),* maelezo ya bidhaa *(product description*) na haki ya kupewa risiti.

iv. Kudhibiti bidhaa bandia katika soko *(anti-counterfeit).*

v. Kufanya utafiti wa masuala ya ushindani na utetezi kwa maslahi ya watumiaji.

103. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kufanya ukaguzi wa mizani, vipimo, vituo vya mafuta, magari ya mafuta, matangi ya mafuta, pampu za kuuzia mafuta na mita kubwa za mafuta *(Depo).* Kwa mwaka wa fedha

2017 – 2018, Wizara ilifanya ukaguzi kama inavyoonekana katika Jadweli Nam. 6 la hapo chini.

Jadweli Nam. 6:
Huduma ya Ukaguzi

Eneo la Ukaguzi	Jumla
Mezani	497
Mita za Depot (Flow Meter)	3
Pampu za kuuzia mafuta	47
Magari ya kusambaza mafuta	6
Bidhaa za Viwandani	3

Chanzo: Wizara ya Biashara na Viwanda, 2018

104. Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji Wizara imefanya ukaguzi wa maduka, maghala, bekari na supermarket ili kubaini ubora wake pamoja na bei za bidhaa hizo kama inavyoonekana katika Jadweli Nam. 7 hapo chini.

Eneo la ukaguzi	Jumla
Maduka	2,148
Maghala	110
Bekari	16
Supermarket	10

Chanzo: Wizara ya Biashara na Viwanda, 2018

105. Mheshimiwa Spika, Katika ukaguzi uliofanyika, bidhaa mbali mbali zenye thamani ya TZS 2.03 milioni zilipatikana zikiwa zimepitwa na muda wake wa matumizi na zilikamatwa na kuondolewa madukani na kuharibiwa. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na vyakula vya makopo, juisi, pempasi na vipodozi.

4.3.3 Programu ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani

106. Mheshimiwa Spika, Program ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani ilitekelezwa na Baraza la kusimamia mfumo wa Utoaji Leseni na Baraza la Taifa la Biashara ambapo ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 502.20 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018. Hadi kufikia Machi 2018, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **TZS 364.31 milioni** kwa ajili matumizi ya kazi za kawaida, Ruzuku na kazi za maendeleo sawa na asilimia 72.54 ya makadirio ya mwaka. Programu ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani ina jukumu la kutekeleza huduma zifuatazo:-

Usimamizi wa Mamlaka Zinazotoa Leseni

107. Mheshimiwa Spika, huduma hii ilitekelezwa na Baraza la Kusimamia Mfumo wa Utoaji Leseni ambalo lilipangiwa matumizi ya jumla ya **Tsh. 250 milioni** kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. Hadi kufikia Machi 2018, Baraza liliingiziwa jumla ya **TZS. 172.58 milioni** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **TZS. 20 milioni** kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 69.03 ya makadirio ya mwaka.

108. Mheshimiwa Spika, Baraza lilijikita kutekeleza majukumu yake katika uwekaji taratibu na udhibiti wa utowaji leseni, kutekeleza mpango wa mapitio ya utoaji leseni,utoaji wa huduma za utawala na uendeshaji wa Baraza pamoja na kutoa ushauri na uhamasishaji kwa wadau.

109. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa taratibu za leseni zinaendelea kuwa rahisi kwa wafanyabiashara, baraza lilifanya vikao vinane (8) na mamlaka zinazotoa leseni pamoja na sekta binafsi kwa lengo la kufanya mapitio na kurahisisha mfumo wa upatikanaji wa leseni. Mapitio hayo ya taratibu za upatikanaji wa leseni yamehusisha sekta nane (8) za afya, elimu, mawasiliano, usafiri, kilimo, uvuvi, mazingira na sekta ndogo ya Biashara ya Dagaa. Baraza lilikaguwa jumla ya mamlaka za utoaji leseni 15 ili kuhakikisha kwamba utaratibu wa utoaji leseni unaendana na Sheria ya kusimamia utoaji leseni na kanuni zake. Aidha, Baraza liliandaa mikutano mitano ya ndani (5) ambayo ilikuwa na lengo la kufanya mapitio ya mfumo wa utoaji leseni ikiwemo kupunguza siku na hatua za upatikanaji wa leseni.

110. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vyema majukumu yake ipasavyo, Baraza imeweka mazingira ya ufanyaji kazi kwa kufanya matengenezo ya ofisi, ununuzi wa vifaa vya ofisi, gari na vespa moja. Aidha, muundo wa baraza *(organization structure)* na mkataba wa huduma *(scheme of service)* umeandaliwa. Wafanyakazi wote wamelipwa mishahara yao kwa wakati pamoja na kuongeza nguvu kazi *(work force)* ya Baraza kwa kuajiri mfanyakazi mmoja katika ngazi ya katibu muhtasi. Jumla ya wajumbe

13 wa Baraza na wafanyakazi wanne (4) wamepatiwa mafunzo yanayohusiana na masuala ya usimamizi, utoaji leseni, ukaguzi, utatuzi wa migogoro na haki miliki. Pia wafanyabiashara wanaotoka katika sekta nane (8) na mamlaka 16 zinazotoa leseni wamepatiwa mafunzo juu ya masuala ya leseni. Katika kutangaza zaidi kazi za baraza, vipeperushi 200 na vipindi vitatu (3) kwenye televisheni vimeandaliwa pamoja na kushiriki katika tamasha la biashara.

Uimarishaji wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

111. Mheshimiwa Spika, huduma hii ilitekelezwa na Baraza la Biashara la Taifa ambalo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilipangiwa matumizi ya jumla za **TZS 202.20 milioni** na hadi kufikia Machi, 2018, Baraza liliangiziwa jumla ya **TZS 110.00 milioni** kwa kazi za kawaida na kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 54.40 ya makadirio ya mwaka.

112. Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Biashara ni jukwaa maalum la majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na lengo lake kubwa ni kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta kuu za uchumi. Hali hiyo ya majadiliano ya pamoja baina ya pande hizo mbili inaleta faida kubwa katika kukuza biashara na utoaji wa huduma hapa Zanzibar.

113. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya baraza, Sheria Namba 10 ya kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara la Zanzibar imepitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuwekwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo tarehe 01, Novemba, 2017.

114. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inathamini mchango wa sekta binafsi katika kujenga uchumi wa nchi. Ili kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi na kuimarisha uwekezaji na urahisishaji ufanyaji wa biashara, Baraza la Biashara la Taifa kupitia mradi wa *"ENGINE - Enabling Growth through Investment and Enterprise Program"* imepata mtaalamu ambae anasaidia katika kujenga uwezo kwa Baraza pamoja na kuweka mifumo mizuri kwa baraza ili kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mtaalamu huyo ameanza kufanya vikao na wadau kwa ajili ya majadiliano ikiwa ni sehemu ya utayarishaji wa Mpango Mkakati 'Strategic Plan' wa Baraza ambao utafuatiwa na mpango wa utekelezaji *(action plan)* wake.

115. Mheshimiwa Spika, Mojawapo ya maelekezo yaliyomo katika Sheria Nam. 10 ya mwaka 2017 ya (ZNBC) ni kuanzisha mabaraza ya Biashara ya Mikoa. Napenda kuliarifu Baraza lako kwamba mabaraza ya Biashara ya mikoa yote mitano tayari yameanzishwa. Na ili kuhakikisha kuwa mabaraza hayo yanatekeleza majukumu yake kwa ufanisi, watendaji wa baraza letu wamefanya ziara ya kukuza mashirikiano baina yake na Baraza la Taifa la Biashara la Tanzania. Ziara hiyo maalum ilikuwa na lengo

la kuangalia jinsi ya uendeshaji wa mabaraza ya Mikoa kwa kutembelea Baraza la Mkoa wa Tanga ambalo ndilo linalofanya vizuri kwa upande wa Tanzania Bara.

Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali

116. Mheshimiwa Spika, huduma hii ilitekelezwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) ambayo ilipangiwa matumizi ya jumla ya **TZS. 507.72 milioni** kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 na hadi kufikia Machi 2018, Wakala iliingiziwa jumla ya **TZS. 420.23 milioni** kwa matumizi yakiwemo ya kazi za kawaida na matumizi mengineyo sawa na asilimia 82.77 ya makadirio ya mwaka.

117. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar *(Zanzibar Business and Property Registration Agency -BPRA)* ina jukumu la kufanya usajili wa biashara na mali ikijumuisha hati za mali ubunifu pamoja na usajili wa nyaraka mbalimbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2017/18 BPRA imeweza kusajili Kampuni 350, Majina ya Biashara 822, Alama za Biashara 281, Jumuiya za kiraia 34 na Nyaraka 3,789.

118. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mradi wa utengenezaji wa mfumo wa kisasa wa biashara *'Business Registration System', BPRA* kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda inatarajia kuzindua mifumo ya kisasa ya Usajili wa Taasisi za Biashara na Usimamizi wa Dhamana kwa Mali zinazohamishika inayotarajiwa kuanza kufanya kazi mwezi Juni 2018 . Kutumika kwa mifumo hiyo kutaiongezea uwezo BPRA wa utekelezaji wa kazi na

majukumu yake katika maeneo yote ya usajili, uhifadhi kumbukumbu na utoaji wa tarifa *(information services).* Wananchi na wadau wengine wa BPRA, popote walipo duniani, watapata huduma za usajili na taarifa kupitia mtandao wa intaneti 'Online Registration Services' na hawatalazimika kufika katika ofisi za BPRA kwa ajili ya kufuata huduma. Napenda kutoa pongezi za dhati kwa kamati ya wataalamu wa ndani kwa kushirikiana na watalamu wa Kampuni ya *"Norway Register Development"* (NRD) kwa kazi ya kusimamia ipasavyo utengenezwaji wa mfumo wa kisasa wa usajili wa biashara.

119. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia BPRA kwa kushirikiana na Shirika la linalosimamia Mali Ubunifu kanda ya Africa (ARIPO), Shirika linalosimamia Mali Ubunifu Ulimwenguni (WIPO) na *"Japan Patent Office"* (JPO) imefanya mkutano wa kitaifa wa kukuza ubunifu na uvumbuzi kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo katika Afrika, taasisi mbalimbali zikiwemo za Serikali, Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), *Karume Institute of Science and Technology,* n.k. Kwa upande wa sekta binafsi, Jumuiya ya Wakulima "JUWA", Umoja wa Wajasiriamali Wanawake *(Women's Entrepreneurship Union),* Chuo kikuu cha Sumait, Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) vilishiriki katika mkutano huo.

Aidha, BPRA kupitia ufadhili wa Shirika linalosimamia Mali za Ubunifu Ulimwenguni (WIPO), kazi ya kuingiza kumbukumbu katika mfumo wa Mali Ubunifu *'Intellectual Property Automation System' (IPAS)* imefanyika kwa kuingiza kumbukumbu za Mali Ubnifu kuanzia mwaka 1919

hadi 2016. Kazi hiyo imefanywa na kampuni ya *"Tryginity"* kutoka nchini Nigeria ikishirikiana na BPRA, kazi hiyo imefanyika kwa muda wa miezi sita kuanzia mwezi wa Novemba 2017 hadi April 2018.

120. Mheshimiwa Spika, BPRA imeendelea kuzifanyia mapitio Sheria ya ufilisi *(Insolvency)* na Sheria ya Usajili Majina ya Biashara Sura ya. 168 ya mwaka 1949 *(Business Names Decree Cap. 168 of 1949)*. Kazi hizo zinafanywa na kamati ya pamoja ya BPRA na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambapo rasimu za sheria hizo ziko katika hatua ya mwisho kukamilika.

4.4 PROGRAMU KUU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA

121. Mheshimiwa Spika, Programu kuu ya Viwango na Tathmini ya Ubora inasimamiwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inajumuisha Programu moja ndogo ambayo ni Viwango na Uthibiti wa Ubora. Programu hii ilipangiwa matumizi ya **TZS 2,483.80 milioni** kwa mwaka wa fedha 2017 - 2018. Hadi kufikia Machi 2018, programu hii imeingiziwa jumla ya **TZS 866.70 milioni** ambayo ni Ruzuku ya mishahara ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo sawa na asilimia 34.89 ya makadirio ya mwaka.

Utekelezaji wa huduma zilizopangwa katika program ndogo niliyoitaja hapo juu ni kama ifuatavyo:

4.4.1 Programu ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora

Uandaaji na Ukuzaji wa Viwango

122. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Viwango imeendelea na jukumu lake la kuandaa viwango ambapo jumla ya viwango 12 vimeandaliwa, viwango 18 vinasubiri idhini ya bodi na 40 viko katika hatua ya rasimu huku lengo la mwaka ilikua ni kuandaa viwango 80 vya Zanzibar. Katika kuendelea na kazi yake ya uchunguzi ili kuhakikisha ubora wa bidhaa, sampuli 59 zimekusanywa na kupelekwa maabara kwa hatua za upimaji wa ubora ambapo bidhaa mbili zilikosa viwango na ubora unaotakiwa na hatua za kuziondosha sokoni zilichukuliwa. Kati ya bidhaa zilizoondoshwa sokoni ni Mafuta ya injini *(engine oil)* lita 12,859 na tende katuni 30.

123. Mheshimiwa Spika, katika hatua za ukaguzi wa bidhaa, Taasisi ya Viwango imefanikiwa kutoa Vyeti vya ubora 1,806 kupitia mawakala wake kwa Ukaguzi unaofanywa nje ya nchi (PVoC). Kati ya vyeti hivyo, vyeti 682 ni vya magari yaliyotumika na vyeti 1,124 ni bidhaa nyengine *(General Goods)* zisizokua magari. Aidha, Taasisi ilifanya ukaguzi wa shehena *(consignments)* 4,893 za bidhaa baada ya kufika bandarini *(Destination Inspection).*

124. Mheshimiwa Spika, Maombi kumi na moja (11) ya matumizi ya alama ya ubora ya ZBS yamepokelewa na kati ya hayo bidhaa mbili (2) zimepatiwa leseni ya matumizi ya alama ya ubora ya ZBS na bidhaa mbili (2) zimepewa cheti kwa mara nyengine *(Renewal).* Ukaguzi katika maeneo

ya uzalishaji ulifanyika ambapo jumla ya bidhaa nne zimekaguliwa ambazo ni Sukari ya kiwanda cha Mahonda, Maji ya chupa ya Super Pure na Crystal Cave kiwanda cha Unga wa Ngano cha *"Zanzibar Milling Corporation"* na Kiwanda cha maji ya Aqua blue *(Zenj Company)* na tatu katika soko Chilli Sauce, Tomato Sauce pamoja na Majani ya Chai "Tabasam Chai".

Aidha, Sampuli 160 zimekusanywa na kupelekwa Maabara kwa hatua za uchunguzi na upimaji wa ubora wa bidhaa hizo na kupatiwa majibu ambapo bidhaa 25 kati ya hizo zilikosa viwango na ubora unaotakiwa.

125. Mheshimiwa Spika, Huduma za uendeshaji wa ofisi zimeendelea kuimarishwa ikiwemo ununuzi wa kompyuta, printa, makabati, umeme, mafuta ya gari, vifaa vya usafi, kukamilisha matengenezo ya Ofisi ya Mkoani na Wete Pemba ambazo zimeanza kutoa huduma na kuwekewa huduma zote za msingi kwa kuweka mazingira mazuri ya kiutendaji, Ujenzi wa kibanda cha walinzi Aman, kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi, na mifumo ya usimamizi katika ofisi. Aidha ZBS imetoa mafunzo kwa Wajasiriamali Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza uelewa wao juu ya viwango na ubora wa bidhaa wanazozalisha.

Uthibiti wa Ubora wa Bidhaa

126. Mheshimiwa Spika, Katika hatua nyingine ya Maendeleo kwa ZBS ni kuanza kazi rasmi maabara mbili ambazo ni maabara ya umeme na maabara ya Nishati ya Mafuta.

Aidha, hatua za manunuzi ya vifaa vya maabara ya Nishati ya Mafuta kwa awamu ya pili yanaendelea na pamoja na kuendelea kwa ujenzi wa Ofisi na Maabara za Maruhubi.

4.5 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC):

4.5.1 Uvunaji na Usafirishaji Karafuu:

127. Mheshimiwa Spika, Shirika katika mwaka wa fedha 2017/18 liliendelea na jitihada zake za utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa Sheria ya ZSTC Nam. 11 ya Mwaka 2011 kifungu Nam. 7(1). Kwa mwaka wa fedha 2017/18, Shirika lilikabiliwa na msimu mkubwa wa vuno la Karafuu ambao haukuwahi kutokea kwa takriban miaka 21 iliyopita. Hata hivyo, Shirika lilifanikiwa kutekeleza jukumu lake la msingi la kununua karafuu kutoka Kwa wakulima bila ya kusita.

128. Mheshimiwa Spika, Shirika la ZSTC lilijiwekea lengo la kununua jumla ya tani 6,770 kwa mwaka zenye thamani ya **TZS 94.7 bilioni.** Hadi kufikia tarehe 31/03/2018, Shirika limenunua jumla ya tani 8,508.45 zenye thamani ya **TZS 118.70 bilioni.** Aidha, Shirika linatarajia kumaliza mwaka kwa kununua tani 8,520 za Karafuu zenye thamani ya **TZS 119.28 bilioni.**

4.5.2 Bei ya kununulia Karafuu:

129. Mheshimiwa Spika, Shirika bado linaendelea kununua Karafuu kulingana na Sera ya Serikali ya kununua Karafuu kwa bei ya asilimia 80 ya bei ya kuuzia nje. Katika msimu

wa mwaka 2017 – 2018 bei ya kununulia Karafuu ilikuwa kama ifuatavyo:-

Daraja la	1	-	TZS 14,000
Daraja la	2	-	TZS 12,000
Daraja la	3	-	TZS 10,000
Makonyo			TZS 1,000

Aidha, Kwa upande wa mauzo ya karafuu, hadi kufikia Mei 2018, Shirika liliuza tani 7,958 zenye thamani ya USD 63.20 milioni sawa na TZS 142.20 bilioni kama inavyoonekana katika Jadweli Namba .. hapa chini.

Jadweli Nam. 8: Mauzo Ya Karafuu Kwa Mwaka Wa Fedha 2017 - 2018

Nam	Jina la Mnunuzi	Idadi ya tani	Thamani US $	Nchi zilipokwenda karafuu
1	Afcom Trading Dmcc	1098	8,759,000.00	India
2	Nomanbhoy $ Sons	4265	33,677,365.48	India na Singapore
3	Din Dayal & Sons	75	642,375.00	India
4	Brooks Trading LLC	170	1,381,190.00	India
5	Tai Eng Pte Ltd	1400	11,002,950	Singapore
6	Catz International BV	100	839,170.00	Holland & UK

Nam	Jina la Mnunuzi	Idadi ya tani	Thamani US $	Nchi zilipokwenda karafuu
7	Mohamed Enterprises	100	830,000.00	India
8	Naushad Trading	100	804,900.00	India
9	Ushachem	200	1,640,640.00	India
10	Dubai	**450**	**3,622,500.00**	Dubai
JUMLA		**7958**	**63,201,323.48**	

130. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Shirika limefanikiwa kuimarisha uzalishaji wa mafuta katika kiwanda cha Makonyo kwa kuongeza siku za uzalishaji kutoka siku 44 kwa mwaka 2015/2016 hadi 178 kwa mwaka 2017/2018 hali iliyopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta ya mimea kutoka Kgs 14,713.6 kwa mwaka 2015/2016 hadi Kgs 59,524.05 kwa mwaka 2017/2018.

4.5.4 Mradi wa Kukuza Biashara

131. Mheshimiwa Spika, Shirika katika kipindi cha mwaka 2017/2018 limeweza kujiimarisha katika soko la ndani na nje hususan katika utafutaji wa wateja ambapo imepelekea kupata wateja wapya wa ununuzi wa karafuu na mafuta ya mimea, vile vile shirika linaendelea kujiimarisha katika ujenzi wa Vituo vya ununuzi wa karafuu, kufanya mapitio ya kazi za Kiwanda cha Makonyo na Tawi la Dar es Salaam, kutangaza bidhaa za Shirika katika Magazeti ya Kimataifa, maandalizi ya Msimu wa Vuno la mwaka wa fedha 2018/19, na pia kuimarisha njia kuu za mapato mengine kwa nia ya kuondokana na utegemezi wa mapato yatokanayo na uuzaji wa karafuu pekee.

132. Kwa upande wa matumizi, Mheshimiwa Spika, Shirika lilikadiria kutumia jumla ya **TZS 10.5 bilioni** ikiwa ni gharama mbali mbali za uendeshaji, wakati matumizi halisi hadi kumalizika kwa miezi tisa ni **TZS 7.1 bilioni.** Matarajio hadi kufikia mwisho wa mwaka 2017/2018 ni kutumia **TZS 10.0 bilioni.** Matumizi haya yanajumuisha vifungu mbali mbali ikiwa ni pamoja na mishahara na matumizi yanayohusiana na mishahara, gharama za matengenezo ya mali za kudumu, gharama nyenginezo za Utawala, ruzuku za Kiwanda cha Makonyo na gharama za masoko.

5 CHANGAMOTO:

133. Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa malengo na majukumu mbali mbali ya Wizara kwa mwaka 2017 – 2018 yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, zipo pia changamoto kama ilivyokuwa kwa bajeti zilizopita. Changamoto hizo ziliendelea kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyopangwa na ufanisi wa sekta ya biashara na maendeleo ya viwanda. Miongoni mwao ni kama ifuatavyo:-

i. Vikwazo visivyo vya kiushuru (NTBs) kwa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar kwenda Tanzania Bara.

ii. Gharama kubwa za kodi na usafiri kwa bidhaa za Zanzibar.

iii. Mazingira ya kufanyia kazi hasa kwa wafanyakazi wetu bandarini ambao wanakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi pamoja na ofisi.

iv. Uwezo mdogo wa uzalishaji wa ndani wa bidhaa na udhaifu wa kutumia fursa za masoko ya kikanda kuongeza usafirishaji pamoja na thamani ya uzalishaji huo.

v. Uwezo mdogo wa watendaji katika kuelewa mbinu za kisasa za uendelezaji wa biashara na viwanda.

vi. Vyama vya biashara na viwanda kupata changamoto ya mageuzi baada ya chaguzi zao za uongozi.

vii. Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozitumia kikamilifu fursa za kibiashara zilizopo katika masoko ya Jumuiya za Kikanda kama vile SADC na EAC na kimataifa kama vile nchi za Ghuba na China.

viii. Upungufu wa Ofisi na wataalam kwa ujumla inaweza kuwa ni kikwazo cha kutekeleza Sera na Mikakati hii mipya.

134. Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zinaweza kutatuka endapo wananchi, Serikali, Sekta binafsi, Jumuiya mbali mbali tutashirikiana katika kupanga na kutekeleza mipango ya kutatua changamoto hizo.

6 PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2018 – 2019

135. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2018 – 2019, Wizara ya Biashara na Viwanda katika utekelezaji

wa majukumu yake imepanga vipaumbele katika maeneo ya ukuzaji biashara, uendelezaji wa viwanda, uwekaji wa mazingira ya kuhamasisha biashara, usarifu wa bidhaa, na usaidizi wa wajasiriamali na wazalishaji wadogo wadogo. Aidha, kazi nyengine ambazo zitapewa umbele ni pamoja na utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa Kusimamia na Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA) na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara.

136. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara kwa Bajeti ya 2018 -2019 vinatokana na dhamira ambayo inataka uchumi wa viwanda kama inavyoelezwa katika ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 kifungu namba 84 (a, b na c) pia maazimio yaliyomo katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III 2017 – 2021) pamoja na miongozo ya viongozi wakuu wa nchi yetu.

137. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Biashara na Viwanda imejipanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2018 – 2019 kama vipaumbele vyake:-

- **Maeneo Tengefu ya Viwanda *(Industrial park)*** **Mheshimiwa Spika**, Wizara ina dhamira ya kuanzisha maeneo tengefu *(Industrial park)* kwa kila wilaya za Unguja na Pemba. Hivyo katika bajeti hii ya mwaka wa fedha 2018 – 2019 Wizara itayaandaa maeneo hayo kwa kuyapima, kuyalipia fidia, kutengeneza ramani pamoja na mpango mkuu wa viwanda kwa maeneo matatu ambayo yatakua tayari

kwa kuanzia ujenzi wa viwanda. Wizara itajenga eneo moja tengefu la viwanda kama ilivyoelekezwa na Serikali.

- **Makao Makuu ya SMIDA**
  Mheshimiwa Spika, Madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa SMIDA ni kuwaweka pamoja wazalishaji wadogo kwa kuwatafutia maeneo, kuwapatia mafunzo na usaidizi wa kitaalam. Hivyo kwa kuanzia, Wizara kupitia Wakala itajenga na kutafanya ukarabati majengo yaliyopo Maruhubi ambapo ndio itakuwa makao makuu. Pia wakala atafanya taratibu za kujenga ofisi na vituo vya kanda/mikoa pamoja na kuimarisha viwanda viliopo ili kuongeza ajira.

- **Kukamilisha Ujenzi wa Maabara na ofisi za (ZBS)**
  Mheshimiwa Spika, Pia katika mwaka huu wa fedha Wizara, inadhamira ya kukamilisha ujenzi wa maabara za Taasisi ya viwango (ZBS) ili kwenda sambamba na ukuaji wa mahitaji ya maabara unaotokana na ongezeko la ujenzi wa viwanda, uimarishaji wa bidhaa za wajasiriamali hususan zinazotokana na usarifu na uongezaji thamani wa matunda, mboga mboga, mwani, asali, chumvi na samaki.

- **Kufanya Utafiti wa Kuimarisha Uzalishaji wa Bidhaa Maalum *(wellness and health products)***
  Wizara ya Biashara na Viwanda kwa kuendeleza

program za utafiti, kwa mwaka huu wa fedha 2018 – 2019 imedhamiria kufanya utafiti ambao utaimarisha uzalishaji wa bidhaa maalum zinatokana na mwani, jamii ya mimea ya asili, viungo na mafuta asilia, bidhaa zinazotokana na kazi za mikono pamoja na nguo *(Craft and Garments)* zenye ubora na zinazoashiria asili ya Zanzibar *(Made in Zanzibar Products).*

- **Kuendeleza Zao la mwani**

  Mheshimiwa Spika, Katika kuendeleza zao la mwani, wizara imekusudia kuendelea kuhamasisha kusarifu na kuongeza thamani zao hili ili liweze kuleta tija. Wizara inatarajia kujenga viwanda cha kusarifu mwani, kwa kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 itajenga viwanda viwili kwa majaribio ya uzalishaji wa *'semi processed carragenean'*. Aidha wizara kwa kushirikiana na *COSTECH* na *TANTRADE* itafanya utafiti wa soko la 'carragenean' ndani ya Tanzania na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili bidhaa zitakazozalishwa zipate soko la uhakika.

- **Kuendeleza Matamasha ya Biashara ya Ndani na Nje**

  Wizara katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2018 – 2019 imepanga kuendeleza matamasha ya biashara ya ndani ya nchi kwa lengo la kushajihisha Biashara na kukuza masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, kuimarisha utoaji wa huduma katika sekta za Serikali na zile za binafsi pamoja na kutangaza bidhaa za wajasiriamali. Vile vile kushiriki katika matamasha muhimu ya nje.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhamira hii, Wizara inakusudia kuiomba Serikali itupatie eneo lililopo Kilimani kwa ajili ya kujenga uwanja wa kudumu wa matamasha mbalimbali ya Biashara, ambapo wizara itahitaji kulipima eneo hilo, kulijaza kifusi, kujengwa mifumo ya barabara, maji, umeme pamoja na kuweka mahema na magazebo ya kudumu kwa ajili ya Maonesho.

- **Kukamilisha mfumo wa usajili kupitia mtandao**
  Katika mwaka wa 2018/19, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) inakusudia kukamilisha mfumo wa uasjili wa biashara na mali kwa njia ya mtandao *(Online Registration System)* ili uanze kutumika rasmi. Mfumo huu utakapokamilika utapunguza muda wa usajili na kuwezesha makampuni ya ndani na nje kusajili kwa njia ya mtandao bila ya kulazimika kufika ofisi za BPRA. Aidha mfumo huu utawezesha kuwa na 'data base' moja tu ya walipa kodi nchini ambayo itarahisisha taasisi nyingine kufuatilia na kuongeza ukusanyaji wa mapato.

- **Majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi**
  Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC) itasimamia utekelezaji wa mabaraza ya biashara ya mikoa kama inavyoelezwa katika sheria na kuandaa majukwaa ya biashara kwa sekta mbalimbali. Mabaraza haya yataongeza wigo wa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kujadili na

kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazoikabili sekta binafsi katika ngazi za mikoa na hivyo kuharakisha uimarishaji wa biashara, viwanda na uchumi hapa nchini.

- **Kutekeleza Mikataba ya Kimataifa ya Biashara Mheshimiwa Spika,** Wizara katika bajeti ya mwaka 2018 – 2019 imeweka malengo ya kuimarisha ushiriki wa Taasisi zetu katika makongamano na matamasha ya kimataifa ili kuzijengea uwezo taasisi hizo na kuimarisha mashikiano ya kikanda na kimataifa katika utoaji wa huduma za biashara, kuweka mazingira mazuri ya sera, sheria, kitaasisi pamoja na kuimarisha uwezo wa ushindani katika biashara za kimataifa na kutanua fursa za masoko na mitaji.

  Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza makubaliano (MOU) na taasisi za kimataifa kwa lengo la kuitangaza Zanzibar katika masoko ya nchi za nje na kuvutia zaidi uwekezaji kutoka nje katika sekta za viwanda, biashara, utalii, kilimo na ujenzi kwa maslahi ya nchi yetu.

  Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeandaa kwa mafanikio makubwa Kongamano *(Forum)* la kwanza la kuitangaza Zanzibar katika soko la China kwa mji wa Shanghai ambapo tumefanikiwa kupata wawekezaji katika sekta za kilimo, uvuvi, ujenzi na uimarishaji wa viwanda na biashara. Makongamano haya yataendelea kufanyika katika miji mingine nchini China. Aidha zipo kampuni nyingine kutoka Marekani

ambazo nazo zimeonyesha nia ya kuingia katika makubaliano kama haya ya kuitangaza Zanzibar katika soko la Marekani.

- **Kitengo cha Mizani na Vipimo: Mheshimiwa Spika,** Wizara itakiimarisha kitengo cha Mizani na Vipimo kwa kununua vifaa stahiki, kufanya ununuzi wa gari pamoja na kujenga uwezo kwa wafanyakazi wa kitengo hicho. Kitengo hiki ni muhimu sana katika kuimarisha huduma za biashara na viwanda na katika ukusanyaji wa mapato.

Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2018 - 2019

138. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ya Biashara na Viwanda imeidhinishiwa jumla ya **TZS 11,363.8 milioni.** Kati ya fedha hizo Jumla ya **TZS 6,663.8 Milioni** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya kazi za kawaida na Mishahara na **TZS 4,700.0 Milioni** kwa kazi za Maendeleo, kama Mchanganuo wa fedha hizo unavyoonekana katika **Jadweli namba 9.**

139. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018 – 2019, Wizara yangu itaendelea kutekeleza program kuu nne (4) na program ndogo kumi (10). Programu kuu hizo kama zifuatavyo:

i. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya BV

ii. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali

iii. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara

iv. Programu ya Viwango na Uthibiti Ubora

6.1 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

140. Mheshimiwa Spika, Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda imegawika katika Programu ndogo tatu kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni kama zifuatazo:

i. Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara na Viwanda;

ii. Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara; na

iii. Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

141. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara na Viwanda ambayo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi itakuwa na jukumu la kutoa huduma ya usimamizi wa rasilimali watu na huduma za kiofisi kwa ujumla pamoja na ununuzi wa vifaa.

Ili kutekeleza majukumu yake, program hii ndogo imepangiwa matumizi ya TZS 1, 709.62 milioni kwa mwaka wa fedha 2018 – 2019.

142. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa program ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ambayo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Mipango,

Sera na Utafiti, itakuwa na jukumu la uandaaji na uibuaji wa sera na tafiti za Wizara, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Wizara pamoja na usimamizi wa takwimu za Biashara na Viwanda.

Katika kutekeleza huduma hizo, programu ndogo ya uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti imepangiwa matumizi ya **TZS 411.62 milioni** kwa mwaka wa fedha wa 2018 – 2019.

143. Mheshimiwa Spika, Program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ambayo inaratibu shughuli za uendeshaji wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya **TZS 496.39 milioni** kwa mwaka wa fedha wa 2018 – 2019.

144. Mheshimiwa Spika, Ili kuweza kutekeleza shughuli zilizopangwa katika Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka 2018 – 2019, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya **TZS 2,617.64 milioni** kwa program hii.

6.2 PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

145. Mheshimiwa Spika, Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali imegawika katika Programu ndogo mbili kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni kama zifuatazo:

i. Ukuzaji Viwanda

ii. Maendeleo ya Ujasiriamali

146. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda itakuwa na jukumu la kutoa huduma ya Uimarishaji wa Sekta ya Maendeleo ya Viwanda ikiwemo kusimamia ujenzi wa maeneo maalum ya viwanda *(Industrial Parks),* Utekelezaji wa SMIDA na kusimamia sekta ndogo ya dagaa, mwani na chumvi ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda.

Ili kutekeleza huduma hii, programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya **TZS 3,665.29 milioni** kwa mwaka 2018 – 2019.

147. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ambayo ina jukumu la kutoa msaada kwa wajasiriamali, Ili kutekeleza huduma hii, programu hii ndogo imetengewa **TZS 166.11 milioni** kwa mwaka 2018 – 2019.

148. Mheshimiwa Spika, Ili kutekeleza majukumu ya Program kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali kwa mwaka 2018 – 2019, naomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya **TZS 3,831.40 milioni** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za programu hii.

6.3 PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA

149. Mheshimiwa Spika, Programu ya tatu itakayotekelezwa na Wizara kwa mwaka 2018 – 2019 ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imegawanyika katika Programu ndogo ndogo nne (4) kama zifuatavyo:

i. Ukuzaji Masoko na Usafirishaji

ii. Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji

iii. Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani

iv. Usajili wa Biashara na Mali

150. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji itakuwa na jukumu la kutoa huduma za uimarishaji wa mazingira mazuri ya biashara pamoja na kuongeza fursa za masoko na urahisishaji biashara ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara.

Ili kutekeleza huduma hizo, programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji kwa mwaka 2018 – 2019, programu hii ndogo imetengewa **TZS 681.80 milioni** kwa mwaka 2018 – 2019.

151. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji ambayo itakuwa na jukumu la kuimarisha ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji kwa kuendelea kutoa

huduma za ukaguzi na uhakiki wa vifaa vya mizani, vipimo, ukaguzi wa biashara na maghala pamoja na ushajihishaji na utoaji wa elimu kwa watumiaji, ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na idara ya Biashara.

Ili kutekeleza huduma hizo, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya **TZS 254.96 milioni** kwa mwaka wa fedha 2018 – 2019.

152. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani itakuwa na jukumu la kutoa huduma za usimamizi wa mamlaka zinazotoa leseni kwa kufanya utafiti na kuweka vigezo vinavyohusu leseni chini ya Baraza la Kusimimamia Mfumo wa utoaji leseni. Aidha, Baraza la Taifa la Biashara litasimamia uimarishaji wa majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuandaa majukwaa mbalimbali ya biashara nchini. Ili kutekeleza huduma hizo zilizopangwa chini ya Programu hii ndogo, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya **TZS 600 milioni.**

153. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Usajili wa Biashara na Mali ambayo itakuwa na jukumu la usimamizi wa usajili wa biashara na mali kwa kukamilisha Mfumo wa kielectronik na kuimarisha mifumo ya usajili wa biashara na mali. Ili kutekeleza huduma hizo, naliomba Baraza lako liidhinishe **TZS 794.7 milioni** kwa mwaka 2018 – 2019.

154. Mheshimiwa Spika, Ili kutekeleza huduma zilizopangwa katika Programu kuu hii ya Ukuzaji na Uendelezaji

Biashara kwa mwaka 2018 – 2019, naliomba Baraza lako liidhinishe **TZS 2,331.46 milioni.**

6.4 PROGRAMU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA

155. Mheshimiwa Spika, Programu kuu ya nne itakayotekelezwa na Wizara kwa mwaka 2018 – 2019 ni Viwango na Tathmini ya Ubora. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imepangiwa kuwa na programu ndogo moja ya Viwango na Uthibiti wa Ubora ambayo itakuwa na huduma za Uandaaji na Ukuzaji wa Viwango pamoja na huduma za Tathmini ya Ubora wa Bidhaa. Utekelezaji wake utasimamiwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS). Ili kutekeleza shughuli zilizopangwa katika programu hii, naliomba Baraza lako liidhinishe **TZS 2,583.3 milioni** kwa mwaka wa fedha 2018 – 2019.

156. Mheshimiwa Spika, Taarifa kamili ya Wizara hii imeelezwa katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (PBB) kwa mwaka wa fedha 2018/2019 – 2020/2021 kutoka ukurasa wa R01-1 mpaka ukurasa wa R01-17.

6.5 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA – ZSTC

Shughuli za Shirika kwa mwaka wa fedha 2018 – 2019

157. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018 – 2019, Shirika la Biashara la Taifa linatarajia kutekeleza shughuli kuu zifuatazo;

i. Ununuzi wa karafuu pamoja na makonyo;

ii. Uimarishaji wa masoko na utafiti;

iii. Uimarishaji wa shamba la Mtakata;

iv. Kukifanyia matengenezo makubwa kiwanda cha Makonyo;

v. Kuimarisha upandaji wa mikaratusi pamoja na miche mengine ya mimea

Ununuzi na Mauzo ya Karafuu

158. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, bei ya kununulia Karafuu kutoka kwa wakulima inatarajiwa kutobadilika kutoka **TZS 14,000** kwa kilo moja daraja la kwanza, **TZS 12,000** kwa daraja la pili na **TZS 10,000** kwa daraja la tatu. Aidha, Shirika linatarajia kununua Karafuu za Kilimo Hai kwa wastani wa **TZS 17,500** kwa kilo.

159. Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Makonyo, kwa mwaka 2018 - 2019, kinatarajiwa kufanyiwa ukarabati mkubwa kwa kubadilisha na kuongeza mashine kwa kushirikiana na kampuni ya 'Kunshan' kutoka China ambayo ndio mnunuzi mkubwa wa mafuta na arki za mimea zinazozalishwa kiwandani hapo. Mkakati uliopangwa ni kutumia shamba la Mtakata kwa kulima mimea inayohitajika kiwandani ikiwemo mikaratusi, michaichai na mirehani. Pia mradi mkubwa utakaowashirikisha vijana wa kulima mikaratusi utatekelezwa. Mazungumzo yameanza na baadhi ya

Wilaya za Unguja na Pemba kuangalia uwezekano wa kupanua mashamba ya mikaratusi ili kiwanda kiweze kuzalisha mafuta kama ilivyo kwenye mkataba baina ya 'Kunshan Aroma Cop. Asia' na ZSTC.

Vile vile ZSTC imepitia taarifa za utafiti wa kuangalia biashara za mazao mengine yakiwemo pili pili manga, hoho, mdalasini, hiliki n.k. ili kuangalia masoko ya ndani na nje ya bidhaa hizo na mpya za kimkakati.

160. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018 – 2019, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Biashara la Taifa limeidhinisha matumizi ya Jumla ya **TZS 78.6 billioni** katika kutekeleza kazi za kawaida na Maendeleo.

7 SHUKRANI:

161. Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Wizara yaliyopatikana ni matokeo ya mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti. Shukrani zangu pia ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi na wajumbe na Makatibu wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na miongozo waliyoitoa katika mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yangu na hatimae kuridhia mapendekezo haya yawasilishwe katika Baraza hili.

162. Mheshimiwa Spika, mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2017 – 2018 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa uliopatiwa Wizara yangu kutoka wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu ikiwa pamoja Kwa madhumuni ya kutambua mchango mkubwa wa Wadau mbali mbali kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje zifuatazo; Jamhuri ya Watu wa China,India,Jumuiya ya Ulaya (EU),USAID, Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Kimataifa la Tasnia ya Malibunifu(WIPO), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), TradeMark East Africa (TMEA), Benki ya Dunia (World Bank),Shirika la Biashara Duniani (WTO),Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola (Commonwhealth Secretariat), REPOA,TANTRADE,Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania (COSTECH),Zanzibar Seaweed Cluster Initiative (Zasci), Milele Foundation, Jumuiya za Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima ya Zanzibar (ZNCCIA) na Wafanyabiashara wote wakubwa , wadogo na Wawekezaji wa Viwanda.

163. Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya Hotuba hii kwa kazi

nzuri waliyoifanya, nawaombea dua njema katika kazi zao.

164. Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wafanyabiashara na wenye viwanda wote wakubwa, wakati na wadogo kwa juhudi zao kubwa za kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia huduma mbali mbali pamoja na bidhaa muhimu za nguo, chakula, vyombo vya moto, na vifaa vya ujenzi. Nawaomba waendelee kushirikiana na Wizara yangu kwa kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuimarisha biashara na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa Spika, tuko katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, hivyo nawaomba wafanyabiashara wote kuwahurumia wananchi na wao kupata malipo yao kwa kuwawekea bei nafuu ili wamudu maisha yao katika mwezi huu.

8 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2018 – 2019

Mapato ya Serikali:

165. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018 – 2019, Wizara yangu imepanga kukusanya jumla ya **TZS 1,513.06 milioni.** Mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio vifuatavyo kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam. 9:-**

Jadweli Nam. 9:
Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018 - 2019

KIFUNGU	MAELEZO	MAKADIRIO
R1146	**Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko**	**1,213,061,000**
1422014	Ukaguzi wa Mezani na Vipimo	110,000,000
1422077	Malipo ya kazi za biashara	1,103,061,000
R0106	**Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali**	
1146002	Ada ya Mali Maiti	1,000,000
1422030	Alama za Biashara	160,310,000
1422031	Uandikishaji wa Makampuni	81,405,000
1422032	Uandikishaji wa Majina ya Biashara	31,155,000
1422034	Ujira wa kutengeneza nyaraka	26,130,000
Jumla Kuu		**1,513,061,000**

166. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa matumizi na ili Wizara yangu iweze kutekeleza programu zake ilizojiwekea kwa mwaka wa fedha 2018 – 2019, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya jumla ya **TZS 11,363.8 milioni** kwa programu nne (4) kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam. 10:**

Jadweli Nam. 10:
Maombi ya Fedha (TZS Mil)

Geresho (Code)	Programu Kuu/Programu ndogo	Makadirio 2018 - 2019 (mil)
PR0101	**Uendeshaji wa Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda**	**2617.64**
SR010101	Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara na Viwanda.	1709.63
SR010102	Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara	411.62
SR010103	Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba	496.39
PR0102	**Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali**	**3831.40**
SR010201	Ukuzaji wa Viwanda	3665.29
SR010202	Maendeleo ya Ujasiriamali	166.10
PR0103	**Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara**	**2331.46**
SR010301	Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji	681.80
SR010302	Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji	254.96
SR010303	Urahisishaji biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani	600.00
SR010304	Usajili wa Biashara na Mali	794.700
PR0104	**Viwango na Tathmini yaUbora**	**2583.30**
SR010401	Viwango na Uthibiti Ubora	2533.30
JUMLA KUU		**11,363.80**

Chanzo: Wizara ya Biashara na Viwanda, 2018

9 HITIMISHO:

167. Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako na wananchi kwa ujumla kwa kunisikiliza.

168. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

10 VIAMBATANISHO

10.1 Kiambatisho Namba1: Mwenendo wa Biashara Zanzibar (2012 – 2017) TZS.M

MAELEZO	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Uagiziaji (imports)	271,273.1	208,051.9	279,552.8	156,941.1	167,088.0	211,413.4
Usafirishaji (exports)	67,390.5	87,799.6	133,587.7	42,407.0	96,234.9	145,756.8
Wingi wa biashara (Volume of Trade)	338,663.6	295,851.5	413,140.5	199,348.2	263,322.9	357,170.2
Urari wa Biashara (Trade Balance)	**-203,882.5**	**-120,252.2**	**-145,965.0**	**-114,534.1**	**-70,853.1**	**-65,656.54**

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, 2018

10.2 Kiambatisho Namba 2: Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara: TZS. (Milioni)

Mwaka	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Kuja Zanzibar	98,871.6	82,906.2	81,384.4	94,650.3	134,059.5	206,482.2
Kwenda Tanzania Bara	224,400.5	501,204.2	366,354.2	401,219.4	84,760.9	33,657.7
Urari wa Biashara	125,528.9	418,298.0	284,969.8	306,569.1	-49,298.6	-172,824.5

Chanzo: Wizara ya Biashara naViwanda, 2018

10.3 Kiambatisho Namba 3: Wastani wa Uingizaji wa Chakula Muhimu katika soko la Zanzibar 2018 (Tani):

Maelezo	Mchele	Sukari	Unga wa Ngano	Jumla
Uingizaji wa Chakula	107,534.0	46,340.0	49,203.0	203,077.0
Matumizi	87,108.0	16,968.0	36,228.0	140,304.0
Bakaa	20,426.0	20,426.0	12,975.0	62,773.0

Chanzo: Wizara ya Biashara naViwanda, 2018

10.4 Kiambatisho Namba 4: Mwenendo wa Biashara ya Karafuu kwa Mwaka 2012 – 2018.

MWAKA	JUMLA TANI ZILIZONUNULIWA	WASTANI WA MANUNUZI KWA KILO	MANUNUZI TZS (IN BILLION)	MAUZO TZS (IN BILLION)	TANI ZILIZOUZWA
2012/2013	1503.3	12439.3	18.7	32.5	2185
2013/2014	5375.4	14008.3	75.3	94.9	5230.9
2014/2015	2826.5	14010.3	39.6	53.3	2766
2015/2016	5764.8	14033.4	80.9	98.2	5667
2016/17	2277	14030.0	31.95	38.4	2253
2017/18	8543.9	14030.0	119.2	140.2	7958
JUMLA	**26290.9**		**365.65**	**457.5**	**26059.9**